The Pursuit of Purity



Christian Lenty, Nick Chilver

Nija ya Usafi

Ufuatiliaji wa Usafi ni rasilimali ya
Pathway to Purity, mpango wa The MST Project.

Hakimiliki © 2024 The MST Project
Haki zote zimehifadhiwa.

ISBN 978-1-4951-8492-5

Toleo la kitabu pepe lilitengenezwa mwaka 2024

Kitabu hiki kimeandikiwa kila mtu aliye tayari kujitolea kufuata usafi wa kingono, ukamilifu wa kiroho, na ukomavu ulio kama wa Kristo.

Shukrani

Safari yangu kuelekea usafi zaidi, ukamilifu, na ukomavu isingewezekana bila neema ya ukombozi ya Yesu, upendo na msaada usioyumba wa mke wangu, na wanaume na wanawake wengi ambao wamepita njia hii pamoja nami.

Christian Lenty

Mungu ana njia ya kutatua mambo ambayo hatuwezi kamwe kuyafikiria. Ninapotazama nyuma, ninaweza tu kushangaa. Kupitia neema Yake alileta wanaume maishani mwangu kunisaidia na nitawashukuru wote daima.

Nick Chilver

Jedwali la Yaliyomo

Ni Nini? pg. 10
Neno Kutoka Kwa... pg. 11

Kipindi cha 1: Hauko Peke Yako pg. 12
Kipindi cha 2: Kufuatilia Usafi pg. 20
Kipindi cha 3: Hakuna Vinyago Tena pg. 28
Kipindi cha 4: Vitundo Vyeupe pg. 36
Kipindi cha 5: Nani Mkufunzi wako pg. 44
Kipindi cha 6: Ipende au Iwache pg. 52
Kipindi cha 7: Jack Kwenye Sanduku pg. 60
Kipindi cha 8: Dhambi, Tubu, Usirudie Tena pg. 70
Kipindi cha 9: Uko Vitani pg. 78
Kipindi cha 10: Watumwa wa Haki pg. 88
Kipindi cha 11: Uhusiano na Giza pg. 96
Kipindi cha 12: Maeneo ya Kijivu pg. 104
Kipindi cha 13: Orodha ya Ukaguzi pg. 112
Kipindi cha 14: Bustani za Uwongo pg. 122
Kipindi cha 15: Kuwa Msimamizi Mzuri pg. 130
Kipindi cha 16: Nguzo za Usafi pg. 140

Kuhusu Waandishi pg. 147
Usomaji wa Ziada pg. 149
Maelezo ya Mawasiliano pg. 151

Ni Nini?

Wanaume wa Kikristo hawako salama dhidi ya mapambano yanayohusiana na majaribu ya kingono, matumizi ya ponografia, na uasherati. Wengi wao hujikuta wakipambana na masuala haya kwa kiasi sawa na kabla ya kumjua Kristo, lakini sasa pia wanakabiliana na aibu ya dhambi zao za siri. Dhambi ya kingono inaathiri afya ya kiroho ya wanaume, afya ya kiroho ya familia zao, na afya ya kiroho ya kanisa.

Tunataka kuonyesha kwa wengine uponyaji na urejeshaji wa Kristo, na kusaidia kuwaongoza wanaume waliovunjika na kuumia katika nuru ya uwazi, toba, na uponyaji. Mwanaume aliyebadilishwa, kuponywa, na kurejeshwa ana vizuizi vinavyoathiri uhusiano na muunganiko wake na Kristo vikivunjwa. Kisha anaweza kuwa nguvu kubwa katika nyumba yake, kanisa, na jamii. Katika mchakato huo, tutaona jinsi Mungu asivyotaka tuishi maisha yaliyozikwa katika aibu. Anataka tupate wenyewe tumaini linalotoka kwa kumjua mguso Wake mwororo na upendo Wake wa huruma anapochanganya vipande vilivyovunjika vya maisha yetu pamoja. Anaulizia tu kwamba tushirikishe na wengine.

Kitabu hiki kimeundwa kubadilisha njia yako ya kufikiri kuhusu usafi wa kingono na ukamilifu wa kiroho - kuathiri jinsi unavyofikiri kuhusu majaribu na jinsi unavyotembea katika utii, na hivyo kukuweka katika njia ya maisha yote ya usafi wa kingono na ukamilifu wa kiroho ambayo itakuongoza kwenye ushindi wa kudumu katika maisha yako ya kila siku.

Neno Kutoka Kwa..

Nakumbuka siku hiyo vizuri sana kwa sababu nilijua kwamba kitu kilihitaji kubadilika katika maisha yangu. Kwa miaka mingi, nilipitia mizani ya usafi; baadhi ya wiki na miezi, nilikuwa imara dhidi ya ponografia, na hata hivyo kulikuwa na nyakati nyingi nyingine ambapo sikuwa imara kabisa. Nilichoka na kwenda na kurudi na hisia ya kutokuwa na matumaini niliyohisi na aibu niliyokuwa nikipitia. Ilikuwa wakati wa kupanga njia mpya kwa maisha yangu, ndoa yangu, na mwendo wangu na Bwana. Na hivyo kulianza safari kuelekea tumaini, msaada, na uponyaji.

Na ingawa safari hiyo haikuwa ya starehe wakati wote, wala haikuwa laini kabisa, imekuwa moja ambayo sijutu. Moyo wangu ni kuwatia moyo wanaume wote kutembea katika nuru na kisha kutoa msaada na mwongozo unaohitajika kukaa hapo. Tunapotaka kufanya mabadiliko katika maisha yetu, tunahitaji kuwa na tumaini kwamba mabadiliko kama hayo yanawezekana. Tunapotaka kutembea njia mpya ya usafi na ukamilifu, tunahitaji kuwafikia wengine kwa msaada. Na tunapotaka kuwa na uhuru ambao tumeutafuta kwa muda mrefu, tunahitaji kupitia uponyaji ambao Kristo peke yake anaweza kutoa. Msaada, tumaini, na uponyaji ni maadili matatu ya msingi yanayochochea Mradi wa MST na maisha yangu.

Unapoanza “kutafuta usafi wako,” tunajitolea kutembea nawe, kukutia moyo, na kukusaidia kuimarisha msingi wako wa kiroho ili uweze kuwa mfano wa usafi na utakatifu katika ulimwengu wa leo. Mifano kama hiyo leo inahitajika zaidi kuliko wakati wowote uliopita. Na kumbuka hili, mahali popote katika Biblia haikusema kwamba kuishi maisha ya usafi kutakuwa rahisi, lakini ni shetani peke yake anayesema haiwezekani.

Christian Lenty

Kipindi Cha 1

Hauko Peke Yako

”Mungu anayekukomboa kutoka kwa uraibu mkubwa zaidi anaweza kukuokoa kutoka kwa majaribu madogo zaidi.” - Christian Lenty

Kuna aina mbili za majaribu ambayo tunakabiliana nayo kama wanaume. Majaribu ambayo yanatukabili na yale ambayo tunayaruhusu wenyewe. Majaribu ambayo tunayaruhusu wenyewe. Mfano wa majaribu ambayo tunaalika ni wakati unapoingia kwenye tovuti yenye uovu. Majaribu yanaweza kukukabili katika shughuli zako za kila siku. Linalokukabili wakati wa mchana na ukakutana na msisimko ambao hukutarajia, ghafla unakumbana na chaguo la jinsi ya kujibu. Wakati ukiwa unakabiliwa na majaribu huwa unachagua jinsi ya kujibu. Umeruhusu majaribu bado una chaguo -chaguo la kuacha, kuinuka, na kutoroka kutoka kwa hali kama Yusufu alivyofanya alipokuwa katikati ya hali ya kujaribiwa (Mwanzo 39). Walakani ni muhimu kukumbuka pia kwamba unapoanza kuweka mawazo yako mateka (2 Wakorintho 10:5) na kuchagua kujibu kwa njia ambayo ni takatifu na ya heshima kwa Mungu, hiyo haimaanishi kwamba adui atakimbia moja kwa moja. Kwa kweli, anaweza kukujia kwa bidii sana kuliko hapo awali. Simama imara (Waefeso 6:10).

Mojawapo ya hila za zamani za adui ni kukata rufaa kwa kile tunachoona kuwa nguvu za kiume na uamuzi ambao hutudanganya kwa kufikiria tunaweza kushinda mapambano yetu sisi wenyewe. Ikiwa bado unafikiria kuwa unaweza kutatua mapambano yako peke yako, basi swali letu kwako ni hili, je, hilo limefanyikaje hadi sasa?

Ikiwa umechoka na mzunguko ule ule wa kutokana na dhambi-kutubu-kurudia kuna jibu. Sehemu ya hilo jibu laweza kupatikana katika jamii kwa sababu kama mkristo muumini, ulifanywa kuwa sehemu ya jamii. Hata kama wanaume wengi wanajua kuwa wanahitaji jamii, kuna vizuizi ambavyo wengi wetu hukubaliana navyo ambavyo vinatuzuia kujenga msingi bora na wa utakatifu unaoturuhusu kutembea na wengine kwa uhuru mkuu na ushindi. Ni vizuizi gani ambavyo vimekuzuia kutokana na kufanya uamuzi ili kuwa makini katika kutafuta uwajibikaji hadi kufikia hatua hii? Ukijifunza kutambua vizuizi, unaweza kujifunza kuvishinda na kujenga msingi wenye nguvu sana. Kuna hatua tatu muhimu za kufuata katika kujenga msingi imara wa usafi wa moyo kudumu:

Kukiri (Yakobo 5:16)

Uhusiano wa karibu (Yohana 15:5)

Mipaka mizuri (Zaburi 15:5)

Hatua zilizo hapo juu zinakuwa na ufanizi zaidi tunapoacha kuishi kama mtaawa/aliyejitenga kwenye kisiwa kisicho na watu na kuwaalika watu kutembea pamoja nasi na kuzungumza maishani mwetu. Lakini tuwe waaminifu, wazo la kujiunga na jamii linaweza kufanya wengi wetu kuhisi aibu, au kutatanisha au kuwa na hisia za aibu au woga kuhusu kushiriki. Hata hivyo, kama wanaume wanaofuatilia utakatifu wa moyo, sote tunahitaji kuwa sehemu ya jamii yenye ufanisi ambapo kuna uwazi na kuhitaji magumu inayohimizwa na kuonyeshwa wazi wazi.

Uhitaji, udhaifu na kufundishika, pamoja na msaada wa Roho Mtakatifu, vinaweza kuwa fadhila ambavyo hututia moyo kutembea katika uhuru na ushindi (Yohana 6:63). Ndiyo maana tunakushukuru kwa kuchukua hatua nzuri ya kwanza na kujitolea kupitia kitabu hiki. Tunapofanya hivyo, tunachagua kuwa wazi wa kuhitaji kila mmoja wetu kuhusu mapambano yetu na majaribu, tamaa, uraibu wa ponografia na dhambi ya ngono.

Unauliza, Je, tunajuaje wakati tumepata jamii yenye ufanisi? Wakati hakuna mtu anayetazamia kukuadhibu kwa tabia yako ya zamani, na badala yake anakuhimiza moyo na kukusaidia unaposonga mbele katika kutembea kwa kina zaidi na Mungu matembezi ambayo yanabadilisha mawazo yako (Warumi 12:2) na kuathiri tabia yake (1 Timotheo 6:11-12). Ukweli wa Warumi 2:1 unapaswa kutupa faraja na amani sote. Hakuna hukumu ya adhabu juu ya hao walio katika Kristo Yesu. Katika Yesu yeye si mwenye dhambi tena bali ni watakatifu na tu warithi pamoja na Kristo (Warumi 8:17) Uhuru unapatikana tunapokaa katika ukweli wake. Utambulisho wetu wa kweli ndani yake. Mungu ni mwaminifu na wa haki na hataudharau moyo uliovunjika na kubondeka (Zaburi 51:17)

Je, unaweza kuwa mtu anayeitikia majaribu kwa njia takatifu na ya heshima? Ndiyo. Je, unaweza kuwa aina ya mtu anayestawi ndani ya jamii iliyo salama na yenye ufanisi? Ndiyo.

Tambua na andika baraka za kutembea katika usafi na utakatifu kama zilivyopatikana katika Neno la Mungu. Weka orodha hii mahali panapopatikana kwa urahisi ili uweze kutafakari juu yake mara nyingi.

Leo, hauko pekee yako tena, pamoja tunajifunza jinsi ya kutembea katika 'usafi' na uhuru zaidi. Hiyo haimaanishi kwamba kutokubaliana na majaribu kama Yusufu alivyofanya zamani sana, lakini ina maana kwamba tutaweza kukimbia hali kama vile alivyofanya. Sisi sote ni wanaume wanaotaka kushinda maswala ya kweli, ambao tumejitolea kutembea na kuishi katika ushindi ambao tumepewa bure kupitia kifo na ufufuo wa Kristo.

Naweza Kuhusiana

Sijambo, asante na wewe? Je, hilo limekuwa jibu lako mara ngapi au jibu ambalo umepewa kwa swali la habari yako? Ilinichukua muda sana kutambua kwamba wakati mwingi sikutaka kuwa mwaminifu kuhusu jinsi ilivyokuwa. Kila mara mimi hung'ang'ana katika jukumu langu kama baba na mume na nimekamilika kabisa katika kuficha mapambano haya kila wakati kujaribu kutayarisha hali ya 'sijambo, ahsante'

Hata niliposhiriki matatizo yangu na Mungu, niliweza kuhisi nguvu yake ikinivuta kuhusu hitaji la kumweleza mtu fulani hapa duniani. Njia za nyenzo safi zilinisaidia kupata ujasiri wa kupingana na kitamaduni na kupinga angavu vya kutosha kutambua na kukubali kwamba sikuwa pekee yangu na kulikuwa na wengine wanaokabiliwa na mapambano kama hayo. Baada ya kuchukua hatua hiyo ya kwanza na kufikia usaidizi na msaada, ninaendelea kukua katika nguvu ambazo zinaweza kupatikana tu katika ushirika na jamii ya KiKristo.

Maswali

1. Je, ni lini wakati wa mwisho ulipoonyesha hali ya ‘sijambo, asante’?

2. Je, ni sababu gani ya msingi unayoonyesha picha hii na kuepuka kuwa wazi kuhusu mapambano yako?

3. Je Mungu anakuambia nini? Je, kuna andiko fulani linalonena nawe kuhusu hili?

Tafakari ya Maandiko

Zaburi 32:2

Zaburi 32:5

Warumi 8

Kipindi Cha 2

Kufuatilia Usafi

“Biblia haisemi kwamba kuishi maisha safi kutakuwa rahisi, lakini ni shetani pekee anayesema hilo haliwezekani.” - Christian Lenty

Je, huwa unaamka na mawazo ya kuwa kuishi maisha ya usafi ni mzigo kupita kiasi? Unaweza kuwa unaishi maisha labda na ukiwa na hofu, kuogopa kwamba leo ni siku nyingine ambayo utatembea kichwa chako kinaning’inia chini, ukitumainia kuepuka mtazamo wowote wa kuvutia ambao unaweza kukujaribu kupitia uwezo wako wa kuzuia. Kwa bahati mbaya kuna wengi wetu ambao ni wenye mtazamo wa kufuatilia usafi kama fursa na sio mzigo. Hilo linawezekanaje? Swali unalopaswa kujiuliza ni “Ninathamini nini?” chochote unachothamini utakifuata na chochote unachofuatilia utaendelea kujitolea kwacho. Muhimu zaidi, swali si tu kuhusu kile unachokifuata heri unafuatilia nani? Mtu huyo anapaswa kuwa Kristo kwa sababu ufuatiliaji wako wa usafi utafunganishwa na ukuaji wako wa kiroho na ukomavu. Safari yoyote ya usafi inayojaribu kuwepo bila uhusiano naye hatimaye hukuongoza nje ya kilima.

Kutafuta usafi unahusu kujitolea kiroho, ambayo na kuchukuliwa muda kwa ajili ya maombi, ibada na kujifunza kwa ukamilifu, lakini pia inajumuisha hatua za vitendo kama vile uwajibikaji wa jamii. Safari yako itakuhitaji uwe mtu wa kufundishika, kujifunza mitazamo mipya, kuwa na ufahamu wa kina zaidi wa maandiko, kutafuta njia za kutumia ukweli wa kiungu, na pia kusitawisha mazoea mapya. Pamoja na kukuza safari yako ya kiroho na kujifunza hatua mpya za vitendo, lazima pia ujifunze kutumia kweli hizi kila siku. Ukuaji na ukomavu wako hautafikiwa kwa njia ya kufikiri kawaida wala kwa kugusa vidole vyako tu. Waebrania 5:14 inatuambia “Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima ambao akili zao kwa kutumiwa, daima zimezoeshwa kupambanua mema na mabaya,”

na Waebrania 6:1 Inasema “Kwa sababu hiyo tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikie utimilifu, tusiweke msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai na wa kuwa na imani kwa Mungu.”

Tunapoingia katika mwenendo wa maisha kufuatilia usafi ni lazima tusalie na ufahamu ya kwamba adui pia anatafuta kutuweka katika hali inayolingana na asili yetu ya kale baada ya viumbe vipya ambayo sisi tuko. (2 Wakorintho 5:17) Kama inavyosema katika 1 Petro 5:8, “Muwe na kiasi na kukesha kwa kuwa adui yenu Ibilisi kama simba angurumaye huzungukazunguka akitafuta mtu ammeze.” Je, hiyo ina maana gani kwako na kwangu? Inamaanisha kwamba kila siku tunakumbwa na adui ambaye ameegemea tu kifo upande wa hisia, uhusiano na kifo cha kiroho (Yohana 10:10). Tunapofuatilia Kristo na usafi zaidi maishani mwetu tunakabiliana na upinzani kutoka kwa adui na kujikuta tunahusika katika vita vya kiroho (Waefeso 6:10-18). Vita vya kiroho sio jambo ambalo tunapaswa kuogopa kutoka kwa woga lakini tunaweza kujiandaa kwa bidii kwa kutambua hatua zake tatu:

Lazima tutambue kwamba adui yuko kazini (Waefeso 6:10-18, 1 Petro 5:8)

Lazima tutambue mbinu za jumla ambazo adui anatumia dhidi yetu (Yohana 10:10, Yohana 8:44)

Lazima tutambue mbinu mahususi ambazo adui anatumia dhidi yetu (Kawaida kulingana na upungufu wetu)

Sisi sote tuna mapungufu na maeneo ya udhaifu. Adui anajua maeneo haya na atajaribu kama awezavyo kuyatumia vibaya kila wakati. Zaidi ya vile meli ya kivita ina ulinzi wa kuzuia mashambulizi ya mbele na nyuma. Ulinzi gani wa kiroho unaofuatilia kwa umakinifu na kutumia mara kwa mara? Leo, unaweza kuanza kuishi maisha ya kufuatilia kwa makini kinyume na majuto tendaji. Je? Hilo linamaanisha wewe au mimi tutakuwa wakamilifu? La hasha! Bila shaka sivyo. Mungu hatuiti tuwe wakamilifu, bali anatuita tuwe watiifu. Ingawa nguvu ya dhambi ilishindwa pale msalabani ni lazima tuchague kutembea katika utiifu wa kila siku.

Usafi sio tu pahali unapoweka macho yako lakini zaidi ya mahali unapochagua kuweka moyo wako. Ufanisi wako katika eneo hili hautegemei tu mipaka unayozingatia bali nia inayotawala ndani yako. Kujaribu kuishi maisha ya usafi inje ya njia za Mungu na matumaini bila shaka kutasababisha kushindwa mara kwa mara. Je, hujachoka kujihisi kuwa unashindwa kila mara? Kama wanaume wanaomcha Mungu lazima tuchukue msimamo na tusiwe na makubaliano pamoja na yale mambo ambayo yataharibu ufuatiliaji wetu wa usafi mkuu na utimilifu. Mungu atatupa neema yake kuishi maisha ya aina hiyo, na tunahitaji kuwaalika wale wanaoishi maisha ya aina hiyo tayari ili wawe mfano kwetu. Hatimaye,

unapoishi maisha haya ya usafi kila mara unaweza kuwa kielelezo ambacho utasaidia wengine kutembea katika nuru na kubaki humo.

Mtindo wa maisha ya usafi na utimilifu utakuhitaji uendelee kusonga mbele la sivyo utajikuta unapiga hatua za nyuma. Hakuna maeneo ya katikati. Unapokuza shauku ya usafi, utaendeleza mtindo wa maisha ya ushindi. Kama wanaume huwa tunafuatilia jambo fulani. Ni lazima tujiulize kila mara," mwelekeo wangu wa sasa unanipeleka wapi?" hakikisha unakoenda ndiko unakotaka kumalizia.

Naweza Kuhusiana

Ilinichukua muda mrefu kugundua kuwa mzigo niliokuwa nimeubeba ulikuwa ishara nzuri. Angalau nilihisi dhamiri yangu ikinitia hatiani kuhusu tabia na mawazo ya maisha. Ushawishi ulianza kukua katika ufahamu ambao niliuthamini kuwa maoni ya Mungu kwangu. Nilijua ananipenda, lakini nilikuwa na hakika kwamba alichukizwa, si ndani yangu, bali kwa ajili yangu. Kuudhika na matokeo niliyo lazimika kubeba aibu, hatia na majuto. Nilijua hivi sivyo ilivyopaswa kuwa. Haikuwa maisha aliyokuwa amekusudia kwa ajili yangu. Lakini pia nilijua kwamba kwa nguvu zangu mwenyewe singeweza kuvunja mzunguko wa dhambi- kutubu na kurudia. Nilikuwa nimechoka sana na pambano hilo. Yesu anaahidi kukata kiu yetu kweli ikiwa tutachagua kutembea naye. Hatua yangu ya kwanza ilikuwa utiifu. Nilijua nilipaswa kufikia kukiri na kuomba msaada, si kutoka mbinguni tu bali pia kutoka kwa wale walio hapa duniani. Kukiri kwa Mungu ni jambo jema lakini unyenyekevu zaidi unahitajika ili kukiri kwa ndugu. Ninapojifunza kutembea kwenye njia ya usafi, Mungu alikuwa mwenye neema na mwaminifu kila hatua ya njia. Alifanya kazi kwa upole ndani yangu kwa kubadilisha pole pole matumaini yangu na nilipomuruhusu anisaidie kukua katika unyenyekevu, nilianza kutambua kwamba kumpendeza Yesu ni fursa.

Maswali

1. Je, uko tayari (Na ujasiri wa kutosha) Kumruhusu Mungu abadilishe matumainio yako?

2. Je, kuna mtu unayeweza kukiri kwake na kama sivyo, unawezaje kupata mtu?

3. Ukishapita hatua hii, unafikiri Mungu anakuongoza wapi?

Tafakari ya Maandiko

Zaburi 101:2-4

2 Timotheo 2:22

Kipindi Cha 3

Hakuna Vinyago Tena

Ni rahisi sana kwa sisi wanaume kujificha nyuma ya lebo na vinyago. Tunapenda kupata lebo zinazotuweka vizuri zaidi au zinazofafanua kile tunachotamani kuwa. Ingawa ni rahisi kutumia lebo hizi kama vinyago kujificha nyuma, hutufanya tuepuke sifa zinazopelekea uhusiano bora na wa uhai kama vile uhalisi, uaminifu na hatari. Je, ni kwa jinsi gani tunatengeneza vinyago hivi? Ukweli ni kwamba kuunda vinyago ni rahisi sana kuliko tunavyofikiri. Mfano unaweza kuwa kiongozi anayefikiri kwa sababu anaongoza wengine, kwamba yuko na hitaji la kuwa mwaminifu na mapungufu, kwa hivyo anaanza kuchukua usafi na uadilifu wake kuwa rahisi. Au kunaweza kuwa na mchungaji, ambaye anahisi kwamba hawezi kuenda kwa mtu yeyote na kushiriki kweli moyo wake na shida. Kwa sababu kama mchungaji, yeye anadhani hapaswi kuhangaika na majaribu au kushughulika na mashaka au kufadhaika.

Labda mfano mwingine ambao sote tunaweza kujilinganisha nao ni mwanaume anayehudhuria kikundi cha wanaume au kifungua kinywa cha wanaume bila kumjua mtu yeyote. Anaweza kuhisi hayuko salama katika mazingira hayo au hahisi uhusiano wowote kwa hiyo anaweka mapambano yake mwenyewe kwa hofu ya kuwa pekee yake, kukataliwa au kunyamazishwa. Mazingira haya pia pamoja na mengine mengi, yanaweza kusababisha kila mmoja wetu kujificha nyuma ya vinyago.

Kwa hiyo watu wa Mungu wanawezaje kujifunza kuishi maisha ya vinyago vya bure? Ingawa tunajua kuwa kujificha nyuma ya barakoa huhifadhi tu picha ya uongo ambao wewe au wengine wamejijengea, lazima tuchague kutoishi katika sura ya mtu mwingine. Tunahitaji kuishi, kufanya kazi na kupumzika katika sura ya Kristo na utambulisho ambao ametupa sisi kama watoto wake (Wagalatia 3:26-27).

Tunapovua vinyago vyetu, tunachagua kutembea katika uaminifu na udhaifu ulio salama katika watu tunaowaamini. Udhaifu wa kweli unapaswa kutupeleka kwenye uaminifu kamili. Ukweli wa kuchagua bado ni uongo mtupu. Udhaifu wa kweli huvunja mtego wa adui na kuleta uhuru wa kweli. Kushiriki maeneo ya hatari na udhaifu hakufungamani na usafi tu au maswala ya ngono; pia ni kuhusu dhambi zetu, kukosa usalama, woga na tunapoleta masuala haya kwenye nuru adui hana cha kushikilia (1 Yohana 1:5-7) Adui anataka kudhihirisha maeneo ya maisha yetu ambayo yanaweza kusaidia kuleta utulivu katika maeneo hayo. Kama wanaume, tunaona ni rahisi kujivunia vipawa tulivyo navyo au ujuzi wa uwezo ambao tumekuza. Lakini wanaume wengi huona ugumu kukiri maeneo yenye udhaifu au mapungufu, na hata kwa umakini sana, wanasitisha kushiriki haya nao wengine na kuomba msaada. Kupuuza maeneo yenye udhaifu au mapungufu, hakushughulikii maswala hayo bali huyaficha hadi wakati ambapo wanaweza kuinua vichwa vyao vibaya tena.

Kutambua udhaifu na upungufu wetu ndani ya jamii salama kama vile kikundi cha wanaume haimanishi kuwa tumeshindwa. Kinyume chake ni ishara ya nguvu ya kweli inayoonyesha sisi ni binadamu, tunahusiana na tunaweza kupokea msaada kutoka kwa waumini wenzetu (Wagalitia 6:2) kutambua udhaifu na mapungufu yetu huturuhusu kutumia kweli za kiroho na kustawisha mipaka inayotumika, hata hivyo kuna vikwazo ambavyo wengi wetu hukubali bila kujua ni nani tunaweza kufikia. Na ni nani ambaye tunaweza onyesha uaminifu na upungufu ikiwa ndugu zetu wengi wanaogopa uhalisi? Je, unashiriki na kila mtu kila wakati na kila mahali? Bila shaka sivyo. Hebu tuzingatie hatua hizi

Pamoja na Mungu (Zaburi 145:18)
Pamoja na sisi wenyewe (Warumi 12:3)
Pamoja na wengine (Methali 27:17)
Wengine wakisaidia kuashiria hali yetu ya vipofu (Waebrania 3:12-13)
Wanaume na wanawake wachache ni kina nani ambao wanaweza kuwa waaminifu na wa kweli? Swali muhimu tunalohitaji kuuliza ni hili; tunawezaje kukua katika ukuu wa kufanana na Kristo ikiwa hatuna nia ya utayari ya kuleta nuru katika maeneo ya maisha yetu ambayo sio. Hayafanani kama wa Kristo?

Ni lazima kwa makusudi tukuze mazingira ambapo watu wote wanaweza kushiriki mapambano yao mahali pa kukataa matukio ya hukumu. Hebu tuchangamkie fursa ya kuja pamoja na watu wasio wakamilifu, kama mimi na wewe. Hii ina maana kwamba tunashughulikia maswala ya kweli. Hatuyapuuzi, kuyatukuza au kuyakimbia chini ya msalaba ndipo msaada unapatikana, tumaini linapatikana na uponyaji unawezekana. Sote ni sawa chini ya msalaba.

Naweza Kuhusiana

Hata ndani ya jamii ya KiKristo mara nyingi tunadanganywa katika kuepuka uhalisi bila kukusudia kuvaa vinyago mbali mbali vya kiulimwengu ni jambo la kawaida katika jamii ya kiulimwengu na hali ya pili kwa wengi. Adui ni mjanja na hajali kidogo kuhusu ni kinyago gani tunachovaa ilimradi tubaki wasio wa kweli. Ilichukua miaka mingi kabla ya kufahamu kwamba nilikuwa bado nimevaa vinyago ili kuunda picha ya uongo. Maandiko yana mengi ya kusema kuhusu picha za uongo na hakuna lililo jema. Nilichokuwa nimeshindwa kuelewa kikamilifu ni kwamba niliumbwa kwa mfano wa Mungu. Imago Dei -mfano wa Mungu nilipewa na Baba yangu wa mbinguni katika tumbo la uzazi la mama yangu. Nilikuwa nikijilinganisha na wale waliokuwa karibu nami na nilikuwa nimevaa hivyo." Vinyago vya KiKristo" vingi vya kutoshea na kuonekana wacha Mungu zaidi kuliko nilivyohisi au nilivyokuwa. Nina utambulisho upya na una mizizi thabiti katika Kristo. Alipoulizwa ikiwa ilikuwa sawa kulipa kodi, Yesu aliuliza sarafu hiyo ilikuwa ya nani naye akajibu, "Mpeni Kaisari vitu vya Kaisari na Mungu vitu vyake Mungu." Umeumbwa kama onyesho la kipekee la kazi ya mikono ya Mungu. Unyenyekevu, uwazi, udhaifu na uhalisi vyote vimo ndani yako na ndiyo enzi ambayo kwayo wengine wanaweza kuona ukuu wa kuumbwa uliyeumbwa kwako. Jivunie kuridhiwa kwako na jinsi ulivyo sasa.

Maswali

1. Je, unajua wewe ni nani ndani ya Kristo au umeshawahi danganywa?

2. Unafikiri ni kwa nini huwa tunaendelea kuvaa vinyago?

3. Je, ni baadhi ya sifa, tabia gani za kipekee ulizopewa na Mungu ambazo zinapaswa kuonyeshwa na unawezaje kuzionyesha kwa uthabiti zaidi?

Tafakari ya Maandiko

Zaburi 30:2

Isaya 44:22

Kipindi Cha 4

Vitundo Vyeupe

“Huwezi kudhibiti dhoruba maishani, lakini unaweza kudhibiti mahali pa kujikinga katikati ya dhoruba hizo. Acha neno la Mungu na ahadi zake ziwe kimbilio lako.” - Christian Lenty

Kuna maoni mengi ya kawaida kuhusu wanaume. Maoni kama vile, wanaume hawapendi kukiri kuwa dhaifu. Wanaume hawapendi kuuliza mwelekeo. Wanaume hawawezi kushiriki hisia zao na orodha ina endelea. Wanachuja njia yao kupitia jamii na kwa mawazo ya kila mtu. Haya yote ni mila potofu ya wanaume na kutenda inje ya dhana hizi potovu kunaweza kuibua maoni kwamba sisi ni dhaifu au kwamba tunahoji uanaume wetu. Kwa hiyo wanaume wengi wanataka kuonekana wenye nguvu na karibu hawalii kamwe. Kwa bahati mbaya wanaishi maisha kana kwamba wanaamini mawazo haya na tunapoyatumia kwa uhusiano wetu na Mungu, inazuia uwezo wetu wa kuwa waaminifu na hatari kwa mapambano na majaribu yetu.

Tunapojaribu kushinda majaribu kwa nguvu zetu wenyewe, tunaweza kuwa na nguvu wakati mmoja lakini hatimaye tunashindwa kwa sababu ushindi hauwezi kushindwa kwa nguvu zetu wenyewe. Hatuwezi kudhibiti majaribu, lakini tunaishi maisha yetu kana kwamba tunaweza na mara nyingi kutafuta hatua za kuzuia pengo. Tunaweza kulinganisha na “vifundo vyeupe” vifundo vyetu huwa vyeupe tunapokunja ngumi kwa nguvu sana hivi kwamba husababisha damu kukimbilia mbali navyo. Ni sahihi kusema kwamba tunapokunja ngumi kwa nguvu sana kupinga jambo fulani, tunajitegemea sisi wenyewe. Taswira iliyo kinyume ya ngumi iliyokunjwa ni mkono uliowazi.

Mkono uliowazi ni mfano wa kukaribishwa, mwaliko wa ombi la usaidizi. Ngumi yetu iliyofungwa inaonyesha upinzani mkali kwa vipengele vya inje. Wakati ngumi yetu imefungwa, hata kama tunajaribu kufanya jambo sahihi kwa kupinga hatuwezi kushika mkono wa yule ambaye amenyoosha mkono wake kuchukua wetu na kutuinua kutoka kwenye makosa yetu. Kuegemea ngumi yetu iliyofungwa hakufai sana kuliko kufungua mkono wetu na kumfikia mwokozi mwenye upendo ambao tayari anakaribia kututolea upendo wake, msamaha wake na neema yake. Ndiyo sisi ni dhaifu bila yeye, lakini haimaanishi kwamba tunapaswa kuanguka katika dhambi. Badala yake lazima tuchague kukimbilia mikononi mwa Yesu.

Mikono ambayo daima iko wazi na tayari kutupokea na kutusaidia kupinga majaribu yanapokuja. Kumbuka Kristo pekee ndiye mwenye nguvu za kutukomboa siku zote.

Basi kwa nini sisi daima tunapinga msaada ambao Kristo hutoa? Ukweli ni kwamba tunataka kuwa katika udhibiti. Lakini katika maisha halisi, mara nyingi tunakumbana na mambo ambayo hatuwezi dhibiti, tunasahau kile tunachohitaji kuwa ni uaminifu kwa hicho. Kama mwanaume, kujaribu kuacha udhibiti katika maeneo fulani inaweza kuwa ngumu lakini ni muhimu ikiwa tunataka kutembea katika usafi zaidi na ukamilifu wa kiroho. Kuna maeneo katika maisha yetu ambayo tunaweza kudhibiti, lakini pia kuna maeneo ambayo hatuwezi.

Hekima hutoka kwa neno la Mungu na uzoefu, ama kujifunza wenyewe au kushiriki nasi na wengine, inatufundisha jinsi ya kutambua tofauti kati ya hayo mawili. Hebu tuanze na kile tunachoweza kudhibiti. Tunaweza kudhibiti matendo yetu, majibu na hisia zetu. Hata hivyo, hatuwezi kudhibiti vishawishi vya inje, watu na hali. Tofauti hii ni pale ambapo wanaume wengi wanaweza kuchanganyikiwa. Mara nyingi, tunajaribu kudhibiti mambo yasiyofaa na kupuuza maeneo tunayopaswa kudhibiti (Wagalatia 5:22-23). Ikiwa tunaweza kudhibiti matendo, majibu na hisia zetu, je kuna jambo lingine tunaloweza kufanya? Ndiyo, ingawa kujifunza kuwa na kiasi ni muhimu na vile tunda la roho, lazima pia tujifunze ni maeneo gani tunaweza kuwa waaminifu kwayo. Tunapoathiriwa na watu au hali ambazo haziwezi kudhibitiwa au wakati majaribu yanaonekana kuwa mengi na tunahisi kama hatuwezi kupinga tena, bado tunaweza kuwa waaminifu katika yafuatayo:

Kutumia zana zinazofaa kwa vita vya kiroho (Waefeso 6:10-18)

Kumwalika Mungu na wengine katika wakati wetu wa majaribu na udhaifu (1 Wakorintho 10:13)

Kutumia neno la Mungu kama upanga wa Roho (Waefeso 6:17)

Zingatia utu wa Yesu (Waebrania 12:1-2)

Kuweka mipaka mizuri (Ayubu 31:1)

Kukimbia majaribu baadala ya kutafuta udadisi usiofaa na usio mtakatifu (Wafilipi 4:8)

Tambua unachoweza kudhibiti (yaani kutafuta maombi, kukataa kuathiriwa na dhambi) na usichoweza kudhibiti (kuondoa majaribu kutoka ulimwenguni). Jifunze kuwa mwaminifu katika unachoweza kudhibiti.

Kwa kuwa waaminifu katika kile tunachoweza kudhibiti, hivi karibuni tutakuza msingi imara. Hii itatuwezesha kusimama imara katika matendo yetu, majibu na hisia yetu tunapokabiliwa na aina yoyote ya majaribu ambayo yanaweza kuwa kichocheo cha uamuzi usiodhibiti afya na zisizo takatifu. Na ingawa Mungu ni mkuu juu ya yote haimaanishi kuwa tunaondolewa jukumu la kibinafsi. Tunaposonga mbele kila siku, na tutafute kuwa mawakili wazuri wa mambo yote, ikiwa ni pamoja na sisi wenyewe.

Naweza Kuhusiana

Uzoefu wangu wenyewe wa vifundo vyeupe hutokea si tu ninapojaribu kwa nguvu zangu kupinga vishawishi bali pia kutokana na kugonga ngumi yangu iliyokunjwa kwenye meza kwa kuhisi kushindwa. Hakika nilikuwa mwanafunzi wa pole pole katika eneo hili na nilikuwa na fursa nyingi za kukuza unyenyekevu na kufanya mazoezi ya kukiri. Nilichoka kumiliki kushindwa kwangu. Lakini kila wakati nilipofanya hivyo, siku zote nilibarikiwa na upendo, subira, ufahamu na kutiwa moyo niliopokea. Nilikuwa katikati ya P2P kabla ya kutambua kwamba ilikuwa katika udhaifu wangu angeweza kudhihirisha nguvu zake. Nilipowaza polepole kuweka tumaini langu kwake na kujifunza jinsi ya kufikia mara tu jaribu lilipoinua kichwa chake, nilipata ushindi wa mara moja. Sasa mkono wangu umefunguliwa huku nikijipongeza mwenyewe, mshauri wangu na Mungu. Ijapokuwa majaribu hayakutuweka, nilipojizoesha kufikia na kuomba msaada nilijifunza kuingia katika nguvu zake. Nilitoka kwenye “Kutubu dhambi na kurudia” hadi “kufikia-kushinda na kurudia.” Katika wakati wa furaha, ya ushindi ikawa tamu sana kuliko tunda lililokatazwa.

Maswali

Je unaona ni vigumu kuomba msaada, na ikiwa ndivyo kwa nini?

Je umedanganywa kwa njia gani?

Je, jamii inajaribuje kuficha udanganyifu unaozungumziwa katika sura hii?

Tafakari ya Maandiko

Zaburi 101:2-4

Kipindi Cha 5

Nani Mkufunzi Wako

“Rafiki wetu wa karibu lazima wawe wale wanaofuata utakatifu kwa sababu watakuwa na matokeo makubwa sana katika maisha yetu. Wewe niambie rafiki zako ni kina nani, nami nitakuambia hasa wewe ni nani au utafanyika kuwa nani. Kimbieni pamoja na wenye haki” - Steven Lawson

Je, unafundishika? Unaweza kudhani ni wewe lakini… ni wewe kweli? Unaruhusu wengine wakuonyeshe mahali pa upofu au huna? Je, unachukua changamoto ifaayo kuelekea ukuaji mkubwa kama dharau au unaona kama kitendo cha upendo na kujali? Ukweli ni kwamba, sote tunahitaji kukuwa na hitaji na hilo hitaji kuwa muhimu mara tu unapofunga ndoa au kuwa na nafasi ya uongozi katika kanisa lako n.k Kwa kweli ikiwa hutabaki kuwa mkamilifu na utakuwa daima kutokana eneo lingine la maisha yako ambalo Mungu anataka kufanyia kazi kufinyanga na kugeuzwa kuwa mfano wa mwanawe Yesu Kristo.

Kwa hivyo tunaweza kukua namna gani? huenda wengi wetu hutazama warsha, kongamano, runinga za mafundisho mtandaoni au zinazouzwa zaidi. Ingawa rasilimali hizo ni nzuri ndivyo zilivyo rasilimali. Kuna wakati tunajaribu kutumia rasilimali kwa maswala ya kiroho. Labda wewe au mtu unayemjua, hufurahishwa na kitabu kipya zaidi ambacho huahidi kitu kulingana na “siku 40 za usafi,” au “miezi 6 kwa uhuru” sehemu ya msisimko inaweza kuja kwa kutiwa na ahadi ya kurekebisha haraka; baada ya siku 40 hutahangaika tena au baada ya miezi sita eneo hili ngumu litaondoka kwenye maisha yako milele. Hata hivyo, marekebisho ya haraka yaweza kutuacha tukiwa tumevunjika moyo na kuvunjika moyo wakati matokeo “yaliyoahidiwa” hayaonekani haraka tunavyotaka, ikiwa yatatokea ukuaji unaobadilisha maisha huja kupitia ufuasi wa maisha marefu, na hapa ndipo tunapotaka kukufundisha kuhusu tofauti kati ya mlalo na wima.

Sisi sote tuko na marafiki. Marafiki tunaoweza kufurahia na kujumuika nao. Marafiki tunaoweza kuwa wazi na waaminifu kwao na ambao tunaweza kusali nao na kutembea nao katika maisha. Hawa wanaitwa marafiki mlalo kwa upande mwingine, ingawa rafiki wima anashiriki vipengele vingi sawa na rafiki mlalo, kuna tofauti. Rafiki wima ni mtu ambaye tumemfungulia maisha yetu na ambaye tumempa haki ya kuzungumza maishani mwetu (Methali 27:17). Tumewashirikisha marafiki hawa wima ili kutupa changamoto katika safari yetu na Mungu hadi kiwango ambacho hapo awali tulifikiria ilikuwa inje ya uwezo wetu. Wanaweza kutaja maeneo katika maisha yetu ambayo hutufanya tukose raha. Wanaweza hata kufichua maeneo ambayo tulidhani tayari tumeshughulikia, hata hivyo tena, tunakabiliwa na ubaguzi wa kuchukua hatua muhimu zinazoongoza kwenye ukuaji wa kweli au kukuta kwamba maeneo hayo labda yapo, tunaweza kudai kwamba wanatuhukumu. Tunaweza hata kujitetea katika majibu yetu kwa changamoto zetu. Ingawa inaweza kuwa vigumu, lazima sote tuwe na marafiki wima katika maisha yetu -rafiki ambaye anajitoa kwa mtu ambaye tunabadilishwa ndani ya Kristo na daima ataelekeza ni kurudi kwa nguvu ya kubadilisha maisha ya neno la Mungu (Waebrania 4:12). Tunawaruhusu marafiki wetu wa wima kusongea karibu nasi na kuona sisi ni nani hasa. Na ingawa hii inaweza kuwa ya kutisha kwa mtu yeyote tu, utaona hivi karibuni ya kwamba marafiki wima hawata kimbia. Sisi sote tunahitaji marafiki kama hao.

Kwa nini sisi tunatumia mlinganisho wa mlalo na wima? Kwa sababu tunapotazama msalaba tunaweza kumuona Kristo katika nafasi ya mlalo na wima, kama mlalo wetu Kristo ni mtu tunayeweza kuongea naye ambaye anaweza kuhusiana nasi (Waebrania 4:15), mtu ambaye tunajua atakuwa pale kwa ajili yetu daima (Zaburi 145:18-19). Kristo ni rafiki yetu, kama rafiki yetu wima, Yesu anaweza kutuonyesha maeneo ya maisha yetu ambayo yanahitaji kuunganishwa na uumbaji mpya ambao tuko ndani yake (2 Wakorintho 5:17).

Utakatifu na haki si tabia ambazo hutujia sisi wenyewe kama kawaida ya watu walioanguka na wenye mioyo isiokombolewa. Ikiwa tunataka kuishi maisha ya utakatifu na ya Uungu, ni lazima tuchunguze kile tunachoruhusu kuingia kwa mawazo yetu, na mioyo pia na wale tunaozungukwa nao (1 Petro 1:13-16). Ndio maeneo tunayohitaji kudumu katika neno la Mungu ili tuweze kusimama imara mbele ya majaribu na mapatano yasiyo matakatifu (Zaburi 119:9). Kama waumini sio tu kwamba tunapaswa maamuzi yetu ya kila siku yaonyesha ukuaji katika eneo la usafi, bali pia tunapaswa maisha yetu yalinganishwe kikamilifu kama Kristo alivyo (2 Wakorintho 3:18). Haya malengo si safari ya siku moja bali ni safari ya maisha yote. Na safari hiyo si ya peke yako, bali ni fursa kwako kuwaalika marafiki wengine. Marafiki ambao Mungu anaweza kuwatumia kuja pamoja nawe na kuwaruhusu kusema ukweli, kuwaonesha neema, kuweka kambi, na kufurahi pamoja nawe unapokuwa katika usafi wa kingono, utimilifu wa kiroho, na ukomavu wa uungu (1 Wathesalonika 5:11).

Mwambie wanaume 1-2 wakubwa wa Kikristo unaowaamini wakuje kukusaidia kukuwa nguzo yako unapoanza kutafuta usafi kwa bidii na kwa uthabiti.

Ingawa wengi wetu wanaweza kufurahia mahusiano ya usawa, mahusiano ya wima yanahusu kufikia na kuomba msaada katika safari hii tuliyoitiwa (Waebrania 12:1- 2). Zaidi ya hayo, tunaweza kujaribiwa kuchagua rafiki wima kulingana na upatikanaji wao na kama ratiba yao inaendana na yetu. Kumbuka kwamba kuna njia bora zaidi ya kuchagua rafiki wima kuliko upangaji wa foleni. Kuchagua rafiki wima kunafaa kuombewa na kuchaguliwa kwa uangalifu sawa na kuzingatia kama mshirika wa maisha au uhusiano mwingine wenye ushawishi. Unapotafuta rafiki wima unauliza mtu kukusaidia kukuwa katika maeneo tofauti ya tabia yako na hali ya kiroho. Huu ni uamuzi muhimu na hupaswa kushughulikiwa hivyo. Leo ni nani unaweza kumualika katika maisha yako kama rafiki wima?

Naweza Kuhusiana

Kuwa na rafiki ambaye ninaweza kushiriki naye mapambano yangu ya kibinafsi halikuwa jambo ambalo niliwahi kufikiria hapo awali na haikuwa dhana niliokuwa naifahamu. Nilijua kwamba nilihitaji kufanya mabadiliko katika njia niliyokuwa nikiishi, na Mungu alikuwa mwenye neema ya kutosha kuniongoza kwa RMPP na nyenzo za P2P. Lakini picha ya kibibilia ya kutembea kwenye nuru haikuwa na maana sana kwangu. Hata hivyo, nilipomaliza kitabu cha nyenzo za usafi, nilitambua kwamba si tu kwamba nilikuwa na rafiki wima, bali pia nilikuwa nikijifunza kutembea katika nuru. Na kadri nilivyozidi kufanya, ndivyo nilivyo zidi kujiona katika nuru. Hatua kwa hatua nilianza kuona maeneo mengine mengi ya maisha yangu ambayo nilihitaji kuleta kwenye nuru na kwa kutii neno la Mungu. Sijamaliza mchakato huu kwa vyovyote na ninatambua asili ya muda mrefu ya kujitolea kwangu. Lakini kila wakati ninapochagua kuendana na ulimwengu wima, ninaanza kupata urafiki na ushirika wa kweli ambao hufanya mabadiliko yanayoendelea kuwezekana.

Maswali

Kwa nini wanaume huona kuwa ni vigumu kutembea katika nuru?

Ni sehemu gani ya maisha yako unafikiri Mungu anaweza kutaka kuangazia nuru yake?

Ni maandiko gani unaweza kutafakari ili kuthibitisha hatua hii?

Tafakari ya Maandiko

Mithali 27:17

1 Wakorintho 11:1

Kipindi Cha 6

Ipende au Iwache

Neno neema, maana yake na jinsi linavyoeleweka linaweza kuwa swala la mgawanyiko wa watu wengi. Andika neno hili katika utafutaji wa Google na umehakikishiwa kupata orodha ndefu ya mawazo, nia, mafundisho na mahubiri mbalimbali. Hata miongoni mwa madhehebu sawa kunaweza kuwa na mitizamo tofauti. Kwa hivyo neema inawezaje kuathiri maisha yako, hasa inapohusu ufuatiliaji wako wa usafi na wa utimilifu wa kiroho? tunaamini kwamba lazima tuone neema kama kitu cha kusherehekea na kutafakari. Wacha tuanze na kusherehekea

Kusherekea

Yesu alikufa msalabani kwa sababu muhimu zaidi kuliko wewe kuketi kwenye kiti cha kanisa kila Jumapili. Alikuja kukuweka uhuru. Fikiria kuhusu hilo: zawadi ya Mungu ya wokovu inakukomboa na kukuweka tofauti kuwa mtoto wa Mungu.

Zawadi yake ya bure ya neema inaweza kubadilisha maisha yako na kukufinyanga tabia yako kuwa mfano wa Mwanawe. Je, hiyo si ya kushangaza na inafaa kusherehekea? Bila shaka! Walakini, unapotazama maisha yako, au ninapotazama yangu, kunaweza kuwa na maeneo mengi ya upungufu na udhaifu. Na ingawa ni za kweli, na pengine hata za kutukatisha tamaa, habari njema ni kwamba hazilingani na Mungu ambaye hajabanwa wala kufadhaishwa na upungufu ama udhaifu wetu. Lakini neema sio tu kitu ambacho tunasherehekea; inapaswa pia kuzaa matunda katika maisha yetu (Mathayo 3:8).

Je, umewahi kutenda dhambi kisha ukatubu haraka uwezavyo? Nina hakika wengi wetu tunayo, na kuwa katika upungufu pamoja nawe, sababu ya mimi kuwa mwepesi wa kutubu mara kwa mara ni kwa sababu nilitaka kujihisi vizuri kuhusu dhambi ambayo nilikuwa nimetoka tu kujihusisha nayo. Je, wewe pia ulijihisi hivyo? kwa hakika, mara nyingi tendo letu la toba linahusu zaidi kusonga mbele kwa haraka kuliko kugeuka kutoka katika uasi wetu.

Hata hivyo, kadiri tunavyokomaa katika safari yetu ya kiroho, ndivyo tunavyoanza kuona kwamba ufahamu wa kina wa neema ya Mungu ni jambo la kutia moyo katika kutembea katika usafi na kuonyesha matunda ya roho (Wagalatia 5:22-24). Tunapoelewa neema ya Mungu na uhuru iliyoleta katika maisha yetu, pamoja na wajibu tulio nao wa kuwa wakili wema wake, tutataka kugeuka kutoka kwa kutokuwa na haki na uchafu wote. Na tunapofanya hivyo, badala yake tutazaa matunda (yaani uchaguzi na matendo) ambayo yanaendana na mtu mpya ambaye tumekuwa katika Kristo (2 Wakorintho 5:17). Mungu hutujalia neema yake zaidi ya vile tunavyoweza kufahamu, na hutuwezesha kuishi maisha matakatifu kwa nguvu zake kupitia Roho Mtakatifu na kwa neno lake. Hii ni neema ya Mungu. Hata hivyo, tunaposherehekea zawadi isiyo stahiliwa ya neema, tunapaswa pia kuchukua muda kulinganisha juu ya gharama kubwa ambayo ililipwa kwa niaba yetu.

Kutafakari

Ni lini mara ya mwisho ulitafakari kuhusu neema? Je, ulinganifu huo ulikuongoza kufikiria juu ya gharama kubwa ambayo ililipwa? Kama tunavyojua sote, ufafanuzi wa neema ni upendo usiyostahili. Neema ni Mungu alitupa kile ambacho hatukustahili (Zaburi 103:10). Dhambi zetu zinastahili adhabu (Warumi 6 :23) lakini Mungu katika upendo wake (Yohana 3:16) alimtuma Yesu kuchukua nafasi yetu msalabani (Warumi 3:21-26). Ikiwa tulikulia kanisani tunajua ukweli huu kwa moyo lakini kwa wengi wetu, tunaweza kupata shida kuelewa jinsi neema inavyoonekana tunapofuata usafi zaidi na utimilifu wa kiroho kila siku. Kwa hiyo hebu tuone kile tunachoweza kujifunza, kutokana na hadithi katika bibilia hasa hadithi ya Yesu katika bustani ya Gethesemani usiku ambao Yuda alimsaliti. Yesu alipokuwa kwenye bustani alikuwa akiomba na kutokwa na jasho la damu inaeleweka kwamba alikuwa akitokwa na jasho la damu kwa sababu ya kufadhaika wakati huo na nyakati ambazo alijua zilikuwa karibu kuja. Kama wewe na mimi tungekuwa katika hali hiyo, tungekuwa tunatafuta kisingizio cha kutofuata au kujaribu kutafuta njia ya kutoroka. Lakini Yesu alisema nini? “Si mapenzi yangu bali mapenzi yako yatimizwe”.

Je, unaona kanuni unayoweza kutumia wakati ujao unapojaribiwa kutembea katika tamaa za mwili wako?

Huyu hapa alikuwa Yesu ambaye, akijua yale yatakayokuja, aliwasilisha mapenzi yake kwa mapenzi ya baba. Kujisalimisha huko kungemgharimu Yesu maumivu makubwa, mateso na hatimaye kifo. Kwa kushukuru, huhitaji kuvumilia maumivu hayo ama kuteseka. Tunaposema hapana kwa mwili na ndio kwa mapenzi ya baba, tunaweza kuhisi kukata tamaa, kufadhaika au usumbufu, lakini ndivyo. Kutembea mbali na majaribu ya dhambi kwenye kompyuta yako, au kwenye bustani, au ofisini n.k, labda hakutagharimu maisha yako. Ijapokuwa haiwezi rahisi, na haungeweza 'kuhisi' kama kuifanya, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu na neema ya Mungu, inawezekana (Wafilipi 4:13).Kumbuka, "Baba, sio mapenzi yangu bali mapenzi yako yafanyike".

Neema ilikuja kwa gharama kubwa na gharama hiyo ilikuwa kifo cha Kristo msalabani. Kifo ambacho kilikuwa cha kuogofya na cha kikatili na bado Kristo alikivumilia kwa ajili yako. Chaguo lako la kutembea katika utiifu kwa neno la Mungu licha ya tamaa za dhambi za mwili wako, ni njia ya kuonyesha shukrani yako kwa zawadi hiyo ya thamani sana (2 Yohana 1:6) Neema ya Mungu ilikuja kwa gharama ambayo usingeweza kulipa wala kustahimili. Neema ya Mungu, kitu ambacho sikustahili lakini kiliwekwa tayari kwa ajili yangu. Gharama ya neema ni kitu ambacho tunapaswa kushukuru, kusherehekea mara kwa mara, kutafakari kwa dhati. Leo maisha yako yanawezaje kusherehekea na kutafakari zawadi hii ya thamani sana?

Naweza Kuhusiana

Kama baba wa watoto watatu, huwa naona inasaidia kutazama uhusiano wangu na watoto wangu ili kuelewa vyema neema ya Mungu na njia yake kwetu. Kwa miaka mingi imenilazimu kuwafundisha watoto wangu mambo yote ninayohitaji kutoka kwao. Kusema tafadhali na asante, bila kuongea na vinywa vyao vimejaa, kuosha mikono yao, kuzima taa, kuweka vitu vya kucheza n.k. Unapata picha. Hata hivyo, jinsi walivyokomaa kuhama kutoka kwa mapenzi yangu kwenda kwa mapenzi yao imekuwa wazi kuwaona wakizingatia sana jinsi kanuni za kiungu zinavyoonyeshwa katika maisha yao, badala ya kila tendo moja ndogo au matendo. Na kwa sababu ninawapenda, kawaida ninawapa neema na matendo yao ninayajua na mioyo yao. Vivyo hivyo, Baba yetu wa mbinguni anaijua mioyo yetu na ana subira nasi. Inafurahisha kutambua ingawa tunapokomaa katika imani yetu, kwa kushangaza tunaitwa kuwa kama watoto –dhaifu na wasio na msaada ambao wanakubali zawadi ya Mungu ya neema na imani rahisi. Hata hivyo, hata kama neema ya Mungu kweli ni zawadi, si kitu ambacho tunapaswa kutumia ili kusingizia mapungufu yetu. Badala yake, tunapaswa kusimama juu ya neema yake ili kutusaidia kusalimisha mapenzi yetu na kutembea katika ushindi wa mapenzi yake kwa maisha yetu.

Maswali

1. Unafikiri ni kwa nini Yesu anatuita tugeuke na tuwe kama watoto?

2. Je, unafikiri kwamba sehemu yoyote ya mapenzi yako kwa ajili ya maisha yako ni kinyume cha mapenzi ya Mungu?

3. Unawezaje kufikiria kuhusu neema ili ikutie moyo kugeuka na kuwa kama mtoto?

Tafakari ya Maandiko

Warumi 6

Kipindi Cha 7

Jack Kwenye Sanduku

“Majaribio ni shetani anayeangalia kupitia tundu la ufunguo. Kujitoa ni kufungua mlango na kumwalika aingie.” - Billy Sunday

Kwa wanaume wengi wanaokubaliana na majaribu ya kila mara, tunafikiri maisha yangekuwa rahisi sana ikiwa mawazo yanayojaribu hayangekuwepo. Ijapokua wazo hilo ni nzuri, katika ulimwengu halisi sisi sote hupata majaribu (Yakobo 1:13-15). Hata Yesu alijaribiwa (Mathayo 4:1, Waebrania 4:15). Tunawezaje basi kuishi maisha ya kukataa mawazo haya machafu, si mara moja au mbili tu, lakini mfululizo, ikiwa tunaishi katika ulimwengu ambapo mawazo ya majaribu hutujia kila mara. Tunapojifunza kutoka sura ya kwanza: kufuatilia usafi tunakabiliana na aina mbili za majaribu. Ikiwa tunakubaliana na majaribu au tunakaribisha majaribu. Daima tunaweza kufanya uamuzi wa kutulia katika matendo yetu, kutafakari ukweli na kuondoka kwenye fursa ya dhambi. Ni muhimu kutofautisha kati ya mawazo na matendo kwa sababu sisi daima tunawajibika kwa matendo yetu.

Labda wewe ni aina ya mtu huyo ambaye anayejitahidi tu na mawazo bila kutekeleza hatua halisi. Ambayo inatuleta kwenye swali. Je mawazo yanayojaribu ni dhambi? Jibu liko kwenye kile unachofanya na mawazo hayo. Je unazishikilia, kuzifikiria, pengine hata kuanza kutamani sana picha au matukio yanayocheza akilini mwako? Ikiwa ndivyo, basi inaonekana wazi kwamba mawazo hayo ni ya dhambi, si takatifu na ya kuvunja heshima kulingana na maandiko (Mathayo 5:28, Marko 7:20-23) au labda unafikiri “lakini hakuna ajuaye ninachofikiria, hivyo hakuna ubaya” jambo ni kwamba Mungu anajua mawazo yako. (Zaburi 94:11, Zaburi 139:2).

Kwa sababu tu hakuna mtu karibu wa kuwajibika kwake haimaanishi hatuwajibiki kwa Mungu. Badala ya kuburudisha aina hii ya mawazo na matukio, tunapaswa kuyakataa moja kwa moja. Kanuni hiyo inasikika kuwa nzuri, sivyo? Kwa hivyo kwa nini inaonekana kuwa rahisi kusema kuliko kutenda?

Labda hiyo ni kwa sababu tunajaribu tu kuzuia mawazo yanayo jaribu na sio kushugulika nayo moja kwa moja. Wazo linalokujaribu linapokuja akilini mwako, haufanyi kazi kulisukuma tu kama mchezaji wa “Jack kwenye sanduku” iwapo ulikuwa kama mtoto, labda ulifurahia kupindisha mshindo polepole hadi, katika muda wa mshangao kutokea mzaha ambao ungetisha nakuleta tabasamu usoni mwako kwa wakati huo. Majaribu ni mengi kama hayo. Tunapitia siku zote bila kujua ni lini majaribu yanaweza kuja. Yanaweza kuja tukiwa kwenye duka la kuoka mikate karibu tena tukiwa tunachukua kiamsha kinywa kuelekea kazini au tukiwa tumekaa katika msongamano wa magari katika saa za haraka sana kuelekea nyumbani. Majaribu hayatakutumia ratiba ya kila siku ya wakati yanapanga kukukabili. Kwa hiyo, tunapaswa kujua jinsi ya kufanya. Mawazo hayo yenye ushawishi yanapokuja katika vichwa vyetu, kujaribu kukandamiza mawazo hayo sio mpango wa maisha marefu ya ushindi.

Kusukuma kidude nyuma chini kwenye kisanduku hakutazuia kurudi nyuma tena. Wakati fulani tulipowasha mpini kwenye kitu chetu cha kuchezea, hatukujua wakati muigizaji huyo angejitokeza.

Ukikandamiza mawazo ya kujaribu, ni swala la muda tu hadi mawazo na matumainio yaliyofichika yatokee tena. Katika kutafuta kwetu usafi, hatuwezi kutibu majaribu ya dhambi kama jeki kwenye kichezeo cha sanduku. Lazima tuyateke mawazo hayo nyara na kuyabadilisha na mawazo matakatifu na ya haki. Ikiwa tunataka kuona ushindi thabiti dhidi ya mawazo yanayo jaribu tunahitaji kuona matukio yetu kama mchakato wa hatua mbili.

1. Hatupaswi kuyaacha hayo majaribu kuenda hivyo, tunayashika mateka (2 Wakorintho 10:5)

2. Ni lazima tubadilishe mawazo hayo na ukweli wa neno la Mungu (Wafilipi 4:8)

Kwa kuongezea, tunaona mpango mkubwa sana wa usafi katika maisha na mawazo yetu, tunapotazama Waefeso 6:10-18. Sehemu hii ya maandiko inatupa amri nane za jinsi ya kujiandaa kwa vita vya kiroho ambavyo tunahakika kuvikabili:

1. Iweni hodari katika Bwana (Mstari 10)
2. Vaeni silaha zote za Mungu (Mstari11)
3. Twaeni silaha zote za Mungu (Mstari 13)
4. Simameni imara (Mstari 14)
5. Mkitwaa ngao ya imani (Mstari 16)
6. Pokeeni chapeo ya wokovu (Mstari 17)
7. Na kuomba katika Roho (Mstari 18)
8. Kuwa macho kila wakati (Mstari 18)

Haya yote ni msimamo thabiti kwa ajili ya vita vinavyoendelea katika mawazo yetu. Haikukusudiwa kuwa katika hali ya kujiandaa kwa mawazo ya kujilinda. Lakini mnaonywa, mkipigana dhidi ya mawazo yanayo jaribu, kama sisi sote tulivyo amrishwa, haimaanishi kwamba adui atatuachilia na kuondoka. Kwa kweli, anaweza kukujia kwa bidii sana. Lazima uwe tayari kusimama kidete katika vita hivi na ujipe moyo kutokana na ukweli kwamba ni vita utashinda katika Kristo kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

Nakumbuka, hata ukiamua kukataa mawazo yenye kushawishi na kutembea katika utakatifu haimaanishi kwamba mwili au hisia zako zitakuwa tayari kutembea katika njia za Roho bila kujali (Wagalatia 5:16-18). Katika maandiko matakatifu, hitaji la sisi kama watu wa Mungu, wasioelewa na walioelewa, ni kusimama imara (1 Wakorintho 16:13, 2 Wathesolanika 2:15, 1 Petro 5:8-9), Kuomba (Waefeso 6:18, Wakolosai 1:11, Wakolosai 4:2, Warumi 8:26) na kuishi sawa sawa na neno la Mungu. (1 Petro 1:13-16, Tito 2:12-13, 2 Timotheo 3:16-17, Zaburi 119:9) Mpaka utambue hitaji la silaha za kiroho na maandalizi thabiti ya kiroho na urejesho, utajipata mwenyewe katika hali ya usafi. Kama watu wa Mungu tukifuata usafi, utimilifu na ukomavu wa kiroho, tuwache kukaa inje katika kucheza na kucheza pembeni na tuwe watu wa vita wanaoweza kuuchukua upanga wa roho na kuishi maisha yanayostahili mwito wetu mbele za Mungu (1 Timotheo 6:11-12).

Vita hivi vya kiroho kwa ajili ya moyo na mawazo yako havitashindwa tu na tamaa yako mwenyewe. Kujitolea kwako au nguvu zako mwenyewe, unamhitaji Mungu na unahitaji vifaa anazokupa. Leo, unawezaje kutegemea Mungu ili kukupitisha katika nyakati hizo za majaribu ambazo una hakika kukabiliana nazo?

Naweza Kuhusiana

Nilijifunza somo hili kwa njia ngumu, nilikuwa katikati ya njia kitabu cha nyenzo za usafi wakati mwana mtindo kutoka kule Ulaya bikini alionekana ufuoni siku moja. Wakati sikuweza kufuta kile ambacho macho yangu yaliona. Nilijua vya kutosha kutoruhusu akili yangu kukaa kwenye kumbukumbu na kujilazimisha kufikiria juu ya kitu kingine. Nilikuwa na furaha mimi mwenyewe. Ilikuwa wiki nyingi baadae nilipokuwa na mkazo na huzuni kwamba taswira ilinijia katika mawazo yangu na majaribu yalikaribia kunishinda. Kama vile wimbo wa AD/DC, 'njia kuu ya kwenda kuzimu'. Hapo ndipo nilipokumbushwa jinsi Daudi (katika zaburi 139) alivyoimba kuhusu njia ya haki kwa mwenye haki. Alimwomba Mungu afunue mawazo yote ya njia mbaya na kumuongoza katika njia ya milele. Alifanya hivyo kwa sababu alijua kwamba dhambi hushikamana na mawazo yetu na inaweza kutuondoa kwenye njia. Lakini neno la Mungu liko hai na lina kazi ya kutosha kuumba kila kitu ambacho kiko, kilicho kuweko na kitakachokuweko na nguvu zake zinaweza kushinda chochote. Itumie kuunda taswira mpya na kumbukumbu mpya ili kuchukua nafasi ya majaribu mawazoni mwako, wakati wowote na popote yanapotokea.

Maswali

1. Je, ni sehemu gani tatu majaribu ya mawazo yanaweza kutoka?

2. Unawezaje kueleza tofauti kati ya hayo?

3. Shiriki andiko moja au mawili ambayo unapanga kutumia wiki hii kuchukua nafasi ya mawazo ya tamaa?

Tafakari ya Maandiko

Wakolosai 3:1-8

Kipindi Cha 8

Dhambi, Tubu, Usirudie Tena

“Toba ni tabia ya maisha yote, si tendo la dakika moja.”
- Sinclair Ferguson

Je, umewahi kuanguka katika dhambi, ukaahidi kutoifanya tena na kisha ukajikuta katika mtindo ule ule wa dhambi siku chache tu baadaye? Ni mzunguko wa kusikitisha na kuhukumika kwa ndani. Wakati wengi tunatenda dhambi, tunaweza kuhisi msukumo wa kina au hata msukumo wa kubadilika, kusema kwamba hatutafanya hivyo tena. Lakini mara tu aibu inapoondoka kama kawaida yetu ya kila siku inarudi kawaida, na wake wetu wanatusamehe n.k, na tutafanya nini? Katika maisha yetu mara nyingi tunaweza kutibu toba kama kitu ambacho tunahitaji kufanya ili kuweza kujihisi vizuri haraka. Kwa kawaida, hatufurahii matokeo ya dhambi zetu, kwa hivyo tutafanya kuharakisha kupitia katika hatua za kukiri kwa Mungu au kumjulisha mmoja wa washirika wetu wa uwajibikaji, ili tuweze kurudi kwenye utaratibu wa kawaida haraka iwezekanavyo. Tunajikuta katika mzunguko wa dhambi-tubu-rudia. Je, inawezekanaje kwa tabia zetu kubadilishwa ambapo tunakuwa aina ya mtu anayetenda dhambi-kutubu na kutorudia tena? Nafikiri hivyo, lakini kwanza inamaanisha nini kutubu? kulingana na ukristo wa sasa toba inafafanuliwa kama ifuatayo: Unapokuja kwenye agano jipya, kuna neno moja unalohitaji kujua, neno la kiyunani metanoia, ambalo kifasihi linamaanisha ‘kubadilisha mawazo’, kutubu kimsingi maana yake ni kubadili mawazo yako kuhusu jambo fulani. Inahusiana na jinsi unavyofikiria juu ya jambo fulani. Umekuwa ukifikiria kwa njia moja lakini sasa unafikiria kinyume. Hiyo ni toba - kubadilika kwa mawazo.

Kama tunavyoona toba ni mabadiliko ya mawazo, lakini je, unahitaji kitu kingine chochote? Unahitaji katika Mathayo 3:8 tumeamriwa kuzaa matunda kulingana na toba yetu. Kutubu ni mwito kwa mfululizo wa matendo na sio tu mtiririko wa maneno matupu. Je, tunawezaje kupata mtindo wa maisha kama huu ambapo tunasonga mbele mara kwa mara katika ukamilifu zaidi, usafi, utakatifu na mfano wa Kristo? Kwanza, ni lazima tuelewe kwamba kwa watu wengi, uchaguzi wa dhambi mara nyingi ni njia ya kukabiliana na maumivu, na uchungu, aibu, upweke, kukataliwa na orodha inaendelea na kuendelea. Kwa bahati mbaya, kuna njia moja thabiti ambayo watu wengi hukimbilia na wanaweza kujipata wenyewe wameshikamanishwa kwa pornografia na dhambi za ngono. Wanaume wengi wanaweza kusema kwamba kwa sababu walikuwa wamechoka walianguka tu katika dhambi. Si kweli, ukweli ni kwamba, ikiwa tulikuwa tumechoka tungekuwa tumeenda kitandani. Hatukuchoka sana kufanya dhambi, lakini tulitumia uchovu wetu kama kisingizio cha kutenda dhambi, Au pengine badala ya kuchoka, tulikuwa “wavivu” na ndio maana tulianguka dhambini. Tena si kweli wengi wetu si wavivu kwa kuwa tunakaa tu siku yote, kutazama runinga, na kula vyakula vingi visivyo na afya. Visingizio visivyo koma kama hivi hujitokeza kama uvivu wa kuchagua. Tunaishia kuwa wavivu katika eneo la maisha yetu ambayo kutokuwa na motisha, kutokuwa na mtazamo, na kutokuwa na kiasi kulichangia kufanya maamuzi mabaya.

Maamuzi ambayo yalivunjia heshima neno la Mungu lililo wazi na kuwaumiza sana wale walio karibu nasi. Mradi tunashikilia aina hizi za visingizio vya kutenda dhambi, tutakosa fursa ya kuona Mungu akifanya kazi katika mioyo na katika maisha yetu (Wafilipi 2:13). Ikiwa nia yako ni asili ya ngono au ya njia za muda za raha ya dhambi ni starehe za uongo. Zinatuibia amani usalama na utimilifu ambao unaweza kupatikana tu katika uhusiano wa karibu sana na Kristo. Wanatuibia nafasi ya kuwa ndani ya jamii ya kiroho ya uwajibikaji na ufuasi. Ni lazima tujifunze kutambua mbinu za kukabaliana nazo ambazo tumekimbilia kwa muda mrefu na badala yake tutengeneze mifumo ya maonyo ya mapema ambayo inaweza kutusaidia kukimbia kutoka kwa tabia tupu na uharibifu. Hatuanguki katika dhambi wala hatulazimishwi kutenda dhambi. Tulichagua kutenda dhambi na kwa sababu tulichagua, sasa tunakabiliwa na ukweli mgumu. Je, bado unapenda mambo ambayo Mungu anasema tuepuke na kuyakimbia (1 Wakorintho 6:18)? Inaweza kuwa rahisi kufikiri kwamba sisi sote tunatatenda dhambi kwa sababu tunaishi katika ulimwengu ulioanguka. Ingawa hiyo ni kweli tusiitumie kama kisingizio cha kuepuka kutazama ndani na kutafuta ni nini na wapi maswala ya msingi yaliyotusukuma kutenda dhambi hapo kwanza. Swali ambalo sote tunapaswa kutafakari ni hili, “Moyo wangu uko wapi (Methali 27:19)?” Ni lazima tutambue kuwa Mungu anataka kufanya kazi mioyoni mwetu, Kuna mfano katika bibilia unaotuonyesha jinsi Mungu anavyotaka kufanya kazi ndani ya mioyo yetu.

Andika malengo yako ya ukuaji wa kiroho kwa miezi 3 ijayo, miezi 6, na mwaka 1. Sasa jiulize kama chaguzi zako za sasa zitasaidia kufikia malengo yako ya ukuaji wa kiroho?

Katika agano la kale, tunaambiwa kwamba Kanaani imewekwa kando kama Mungu alivyoahidi urithi kwa wana wa Israeli. Kanaani ilikuwa nchi inayotiririka maziwa na asali. Kwa bahati mbaya, hata kwa ahadi hii, wana wa Israeli bado walitamani maisha yao ya zamani huko Misri. Je, unaona ulinganifu hapa kutafuta kwetu usafi zaidi katika ulimwengu wa mashambulizi ya mara ngono ya wazi na kila mara kwa mara? huenda usiishi Misri tena “Yaani pornografia, dhambi ya ngono” lakini ‘bado unaweza kutamani nchi ya utumwa.’ Kama watu wa Mungu wanaofuatilia usafi, na kutamani nchi ya Kanaani: mtindo wa maisha thabiti wa ukuaji wa kikristo kupitia neno la Mungu, jamii ya kiroho, maombi yaliyokomaa thabiti, kusoma maandiko, kuabudu na kufunga. Tunapowekeza katika nchi mpya tuliyomo ni lazima kila wakati tuweke ahadi ya kutupa masalio ya mwisho ya nchi yenye tumetoka (Waebrania 12:1). Kuwekeza muda kwa ajili ya ukuaji wa kiroho siku zote kutalipa kwa sababu kutakupa uwezo wa kuishi maisha ya kupinga au kushinda dhambi. Sio kwa sababu ni lazima, lakini sababu unataka. Sio kwa sababu ulirekebisha tabia yako, lakini kwa sababu Mungu alibadilisha moyo wako. Si kwa sababu unapenda dhambi nyingine, bali kwa sababu unampenda Yesu. Leo, unawezaje kuchukua toba yako na kuitia motisha ya mabadiliko ya maisha marefu?

Naweza Kuhusiana

Nilikuwa na miaka mitano katika maisha yangu ya kikristo kabla Mungu hajaanza kunionyesha kwamba bado nilikuwa ninaishi katika ‘nchi ya utumwa’. Ndio, nilikuwa na tamaa mpya na tabia mpya, lakini pia nilikuwa na nyingi za zamani. Njia kuu akilini mwangu bado ilikuwa wazi na kuweza kuchukua athari zake kwenye uso wangu. Kutumia muda katika mambo ya Mungu ni sehemu muhimu ya safari ya Mkristo yeyote jinsi yalivyo tu kwa kufanywa upya nia zetu ndipo tunaweza kujisalimisha kwa mchakato wa kugeuzwa. Mawazo yangu yalipoanza kushikana na ukweli wa neno lake, moyo wangu wa jiwe ulianza kulainisha sauti yake katika Warumi na mwororo kama udongo mwepesi. Nilianza kukumbatia imani katika moyo wangu na kuleta vita hivi kwake na mshirika wangu wa uwajibikaji. Aibu niliyokuwa nimeificha hapo awali ulibadilishwa na uhuru na furaha ambayo nililazimika kushiriki tu. Toba ni mawazo yangu mapya na njia panda ya njia ya milele.

Maswali

1. Je, umepata kuhukumika katika eneo gani hivi majuzi?

2. Je, haiwezekani kuweka katika matendo yale usio yakubali kwa mawazo yako. Je, unakubali/hukubaliani na kwa nini?

3. Ni hatua gani zinazofaa unazoweza kuchukua ili kubadili jinsi unavyofikiri kuhusu maeneo haya ambayo unahisi kuhukumika/kushawishika?

Tafakari ya Maandiko

Mithali 26:11

1 Yohana 2:3-6

Kipindi Cha 9

Uko Vitani

***"Hakuna haja ya kuwa na huruma, upole au usahihi wa kisiasa unaposhughulika na adui."* - Christian Lenty**

Katika vipindi 8 vya kwanza tumejifunza kuhusu zana za vitendo tunavyoweza kutumia kutafuta usafi wa kila siku. Katika vipindi 8 vifuatavyo, tutakuwa tunajifunza kuhusu mtazamo na zana za kiroho zinazohitajika tunapotafuta kuhamia mtindo wa maisha ya uhuru na ushindi. Kutembea katika uhuru huo na ushindi, ni lazima kwanza tutambue kwamba tu katika vita vya kiroho na kuwa vita vipo kila wakati iwapo tutachagua kuvitambua au la (Waefeso 6:12). Ingawa hatuwezi daima kuona vita vya kiroho ambavyo biblia inazungumzia kuhusu kama tungejivunia kwenye sinema ya vita, vipo vinaendelea. Kwa hivyo, ni mojawapo ya vipengele vyenye changamoto sana za imani na safari yetu ya kila siku. Tunajuaje tuko katika hatari ya mashambulizi kutoka kwa adui au wakati tunapata siku mbaya tu au tunashughulika tu na matokeo ya asili ya matendo yetu wenyewe? Ukweli ni kwamba, hivi vitu vyote hufanyika wakati hatuamini kwamba shetani na mapepo yake wamejificha nyuma ya kila kichaka wakingoja kutupiga katika kila jambo kuu au la kawaida, tunajua kwamba biblia inasema kwamba Ibilisi huzunguka zunguka akitafuta mtu ambaye anaweza kummeza (1 Petro 5:8). Picha hii ya kishenzi ni ngumu kupuuza. Kwa hiyo ni lazima tujifunze jinsi ya kupigana vita hivi vya kiroho na kukumbuka kwamba sisi sio tu wanyonge kwa ajili ya mnyama mwenye njaa. Katika Kristo sisi ni wapinzani wa kutisha (2 Wathesalonika 3:3)

Acheni tupitie tena (1 Petro 5:8) inayotuambia kwamba kwa kuwa mshtaki wenu Ibilisi kama simba angurumaye huzunguka zunguka akitafuta mtu ambaye aweza kummeza. Sasa tunataka uzingatie neno moja kati ya hii. Huzunguka zunguka kamusi inafafanua neno kuzunguka kuwa ni uwindaji na wizi na hizi maana zinatupa uwazi ya jinsi adui anavyofanya kazi na asili ya vita vyake. Kuna nyakati ambapo majaribu na mbinu zake huwa wazi na zinaonekana, lakini kuna nyakati zingine yeye hungojea kwa subira muda mwafaka wa kushambulia. Wakati unaweza kuwa na uchovu, kuchanganyikiwa, kuchoka kabisa kwa kweli inaweza kutoka wakati wowote. Hata hivyo, ingawa tunamfahamu adui, tunachagua kubaki tukimtazama Kristo. Ikiwa tutakuwa thabiti katika kumwalika Kristo katika kila kipengele cha maisha yetu, basi atakuwa mwaminifu kutusaidia kukabiliana na chochote kitakachotupata, iwe ni matokeo ya matendo yetu wenyewe au mashambulizi ya moja kwa moja kutoka kwa adui. Mkakati huu si mbinu wa kupita kiasi. Ni udhalishaji wa kila upande unao mruhusu Kristo kurejesha, kuponya na kutulinda. Na ikiwa tumerejeshwa, kuponywa na kulindwa na Kristo, basi hatuhitaji kuishi kwa uoga; haimaanishi kuwa hatuwezi kujaribiwa au kutenda dhambi tena, lakini inamaanisha kuwa sisi sio bata aliyekaa asiye na uwezo wa kungoja kifo tu. Pia huondoa fursa yoyote ya kutoa visingizio. Hatuwezi chagua kutenda dhambi na tunasema “shetani amenisukuma kwa njia yake ifaayo.”

Ikiwa kwa kweli tunamruhusu Mungu kulinda nyanja zote za maisha yetu, basi lazima pia tuchukue jukumu la wakati tunapochagua kuacha ulinzi huo na kuchagua dhambi badala ya uhusiano wetu na Kristo. Kama waumini, sasa tuna uwezo wa kuona ulimwengu, uchaguzi wetu na watu wengine n.k kupitia hali ya kiroho (2 Wakorintho 3:16, Matendo 26:18). Macho yako yamefumbuliwa na unaye Roho Mtakatifu anayekaa ndani yako. Huoni tena ulimwengu kupitia macho ya kupuuza; sasa unaona ulimwengu kupitia ufunuo na uamsho wa roho yako. Muulize Mungu akupe ufahamu mkubwa zaidi wa kiroho na mtazamo wa ulimwengu huu na vita vya kiroho ulivyo ndani. Umewahi kusikia au kuona kitengo cha kijeshi kikiingia kwenye vita bila kujiandaa na bila silaha zinazohitajika kushinda vita? Bila shaka hapana kama askari katika jeshi la Bwana (2 Timotheo 2:4) Tuna vifaa vya kiroho vinavyohitajika ili kutembea katika njia za usafi na utakatifu kulingana na neno la Mungu. Jambo moja ambalo tumeona miongoni mwa wanaume ni mwelekeo wa asili yakutaka kupigana vita kwa kutumia silaha za mwili, badala ya zile za kiroho. Zana/silaha halisi ni pamoja na kuweka vichujio, kuwa na washirika wengi wa uwajibikaji wenye kupiga simu, uharaka na kuwa na mipaka mizuri inayotuzunguka, ndani na katika hiyo hakuna hata moja ya haya ambayo ni mbaya. Lakini hizi zana/silaha za kimwili na ingawa ni nzuri, tuko kwenye vita vya kiroho.

Maswala ya kiroho yana suluhisho moja tu: ya kiroho kama Glen's Spaundling anavyosema "Chakula cha kiroho hukupa nguvu kwa ajili ya vita vya kiroho". Kumbuka hilo katika Kristo:

- Tuna urafiki na Mungu
- Roho Mtakatifu anakaa ndani yetu na kufanya kazi ndani yetu,
- Tunaweza kutumia neno la Mungu kama silaha dhidi ya mawazo ya kujaribu
- Tunaweza kupata maombi kila siku na tunaweza kuwa na imani kwamba Mungu anasikia maombi yetu
- Tunaweza kuliita jina la Yesu, jina lipitalo majina yote
- Tunaweza kujifunza kutoka kwa maisha yetu ya zamani na kufanya uchaguzi mpya kulingana na utu wetu mpya

Huenda umesikia msemo usemao, "Usimpe shetani nafasi kwa sababu atachukua hatua kubwa" lakini kwa nini tuhangaikie kile tunachompa shetani? Kama waumini na watu wa Mungu, tunapaswa kuhusika sana na kile tunamtolea Mungu. Tunapokuja kwa Mungu na kumpa nafasi ya kutukomboa kutoka kwa majaribu, yeye daima atajidhibitisha kuwa mwaminifu (1 Wakorintho 10:13). Hii ni ahadi ya Mungu na kila wakati yeye hutimiza ahadi zake. Kuzungumza kuhusu vita vya kiroho kunaweza kuwa mada isiyofaa, lakini ni mada ambayo inazungumziwa katika biblia na ambayo Paulo anatuhimiza tujitayarishe kwa ajili yake (Waefeso 6:10-18). Ukweli ni kwamba, tulijitolea kwa ajili ya vita hivi tulipofanya uamuzi wa kumfuata Kristo kama Bwana na mwokozi.

Tabia zetu kuelekea kipengele hiki muhimu sana cha kiroho, ni muhimu, na hujalisha sana. Hatupaswi kuruhusu kudanganywa katika kuamini kwamba kwa sababu hatuwezi kuona vita vya kiroho au wale wanao vipiga vita ambavyo si ya kweli kabisa, ni hivyo na ni hatari kubwa sana. Kuna watu katika maisha yako ambao wataathiriwa na kutaka kwako kwa kupigana dhidi yake, au kutotaka kwako kufanya hivyo.

Naweza Kuhusiana

Kwa kuzingatia njia ya uovu, shetani na mapepo kawaida huonyeshwa kwenye runinga, ni rahisi kukataa nguvu za kiroho kama fantasia. Na hivyo ndivyo tu adui angependa tufanye, kutupilia mbali wazo na kutozingatia vita vya kiroho. Kama vile dhambi ilizaliwa kutokana na tamaa ya ubinafsi katika bustani la Edeni, tamaa zetu za ubinafsi ndizo shetani hutumia kuathiri maamuzi tunayofanya. Mara macho yangu yalipofunguka na kuanza kuona kwa macho ya kiroho, nilianza kutambua tabia ambazo mwili wangu ulikuwa umejengeka kwamba zilikuwa zinanifanya nishindwe. Unapofanya uamuzi wa kufuata usafi, unaanza kuona uwezo wa uharibifu ambao tabia hizi zinao. Na unapochagua kutazama Kristo na yeye anakuwa mtazamo wako, yeye ni mwaminifu daima ili kukuweka katika kutembea kwako na kukuongoza dhidi ya yule muovu. Wazia mguu wako ukiwa nyuma ya shingo ya shetani wakati wowote tabia yako inapokuwa ya uwindaji na kutazamia yale ambayo Kristo tayari amefanya.

Maswali

1. Ni silaha gani za kimwili unazoziona katika vita vya usafi na ni silaha gani mpya za kiroho unaweza kutumia badala yake?

2. Fikiria juu ya moja ya tabia zako za kimwili na ueleze jinsi vinavyo jikita katika ubinafsi?

3. Je, ni hatua gani unaweza kuchukua ili kuanza kusitawisha mazoea ya kumheshimu Mungu na ni nini kinakuweka kuzitumia?

Tafakari ya Maandiko

Waefeso 6:10-17

Kipindi Cha 10

Watumwa wa Haki

“Kujua wewe ni nani kama mtoto wa Mungu ni muhimu kwa ukuaji wako katika Kristo na kuwa mtu ambaye Mungu amekusudia uwe. Hakuna mtu anayeweza kuendelea kuishi kwa njia ambayo haiendani na kile anachoamini juu yake mwenyewe.” - Neil T. Anderson

Kabla ya kuingia katika uhusiano na Kristo, pengine hatukuelewa kwamba tulikuwa watumwa wa dhambi (Warumi 6:17). Tunapojihusisha na dhambi ya kurudia-rudia, huenda tukafikiri kwamba tunaburudika, lakini kwa kweli tuliishi kuwa na aibu, hatia, na majuto zaidi kuliko tulivyowazia au kuafikiana. Au labda hatukuona jinsi tulivyochanganyikiwa hadi tulipoingia katika uhusiano wa kubadilisha maisha na kubadilisha moyo kwa mahusiano ya mwokozi wetu. Mara tulipokubali msamaha wa Kristo kupitia kazi yake msalabani, tulifanyika wana wa Mungu (Wagalatia 3:26) na tuliitwa kutembea katika utakatifu na haki (Waefeso 4:23-24). Na habari njema ni kwamba Mungu hatuoni tena kuwa wenye dhambi bali watakatifu (Warumi 5:1,1 Petro 2:9). Hata hivyo, kwa sababu sisi si watumwa wa dhambi tena na sasa tu watumwa wa haki (Warumi 6:17-18), haimanishi kwamba kwa ghafla tumekuwa wakamilifu na jaribu na dhambi zimetoweka kabisa.

Kwa hakika, bado tunaweza kujipata tunachagua kutenda dhambi kwa njia zinazolingana zaidi na mtindo wetu wa maisha ya zamani kabla ya kumpata Kristo. Ukweli ni kwamba, dhambi inapunguza usikivu wetu kwa Kristo na Roho Mtakatifu na ikiwa tunashikilia dhambi ambayo haijaungamwa, inampa adui nafasi ya kutulisha uongo kuhusu utambulisho wetu wa kweli.

Swali ni je, tunawezaje kutembea kwa mtindo wa maisha tofauti na uliotajwa hapo juu au ule unaoweza kujikuta umekwama ndani leo? Yote huanza kwa kuelewa kwamba sisi sote ni 'watumwa' wa kitu fulani. Sisi sote tunafuata mtu au kitu. Hakuna mtu anayeendesha maisha bila aina flani ya mwongozo. Na kwa sababu sisi ni viumbe kipya ndani ya Kristo haimaanishi kwamba sisi ni viumbe vilivyokomaa tayari. Ukomavu huja kwa kufanya maamuzi mazuri kila mara yanayo mheshimu Mungu na neno lake na kulinganisha uumbaji mpya tuliyomo ndani ya Kristo (2 Wakorinto 5:17).

Kufanyia kazi utambulisho wetu mpya kutatuhitaji tuache mazoea yetu ya zamani - mazoea ambayo yalikuwa ya kustarehesha na ya kufurahisha miili yetu, lakini yenye dhambi na yenye madhara kwa roho zetu. Inatubidi kwenda kwenye neno la Mungu ili kujifunza jinsi ya kuishi maisha haya mapya tuliyo nayo ndani ya Kristo. Maandiko hayatuambii tufanye tunachotaka; Amri za Mungu zimekusudiwa kutuongoza katika yote aliyo nayo kwa ajili yetu. Njia zake hazikusudiwi kututawala bali kutulinda. Hivyo ndivyo baba yetu mwenye upendo anatufanyia sisi watoto wake, Mungu anataka kutulinda kutokana na ushawishi na uharibifu wa dhambi. Kama wanaume wanaofuata usafi na utimilifu, kuna maeneo tatu muhimu ya maisha yetu ambayo tunapaswa kufahamu ili tusirudi nyuma katika asili yetu ya zamani na tabia zake.

Kihisia

Ikiwa tunachagua tabia ya dhambi isiyotubu, basi tunachagua kidogo kuliko bora ya Mungu kwa ajili yetu linapokuja swala la hisia na dhamira zetu. Kuchagua vitendo vya dhambi hakutachangia mahali pa afya ya kihisia. Badala yake, tunaweza kushindwa na hisia za aibu, kulaaniwa, hatia, wasiwasi, kutojistahi n.k Kama watu wa Mungu na watoto wake, tunahitaji kukata na kugeuka kutoka kwa vitendo kama hivyo ambavyo hualika hisia na dhamira zisizofaa na zilizo tofauti.

Kiroho

Ikiwa tumechagua tabia ya dhambi isiyotubu. Basi tunachagua kidogo kuliko bora ya Mungu kwa ajili yetu linapokuja swala la hatua zetu za kiroho, hakuna aliyestawisha uhusiano wa karibu zaidi na Mungu huku aking'ang'ania dhambi na usherati. Badala yake, kuna uwezekano kwamba mwenendo wa mtu wa kiroho utateseka ikiwa hautageuka moja kwa moja kuwa ngumu na baridi wakati maamuzi ya dhambi ya kurudia-rudia yanapoendelea kukita mizizi na kukua. Kama watu wa Mungu na watoto wake, tunahitaji kukataa na kugeuka kutoka kwa matendo kama hayo ambayo yataleta kifo kwenye safari yetu ya kiroho.

Kimwili

Ikiwa tutachagua tabia ya dhambi isiyotubu, basi tunachagua kidogo kuliko bora ya Mungu kwa ajili yetu tunapokuja kutoka katika hali yetu ya kimwili.

Kuendelea kuchagua tabia ya dhambi kunaweza kusababisha kukosa umakini kazini, mahusiano nyumbani na hata kukosa usingizi usiku. Kama watu wa Mungu na watoto wake, tunahitaji kukataa na kugeuka kutoka kwa matendo kama hayo ambayo hualika mfuko wa kibinafsi.

Hata hivyo ni muhimu kuelewa kwamba maisha ya utakatifu hayaji kwa kubadilisha tabia zetu, lakini kwa kuamini sisi ni nani ndani ya Kristo Yesu. Tunapokumbatiana na mtindo wa maisha ya utakatifu na haki (maisha yetu mapya), na tunakataa tabia za dhambi (maisha yetu ya kale). Wakati unakubali chaguo moja, unakataa chaguzi zingine zote. Na kwa sababu unaweza kuwa ulijitoa kwenye mzunguko wa uharibifu wa dhambi jana, haimanishi kuwa Mungu hawezi anza kukuweka huru hapo na hapo. Wewe mfikie tu na atakujibu.

Kama neno la Mungu linavyosema wazi, wewe si mfungwa wa dhambi tena; wewe sasa ni mtakatifu ambaye anajifunza jinsi ya kutembea katika utakatifu licha ya kuwepo na dhambi pande zote. Kristo alikuvisha na haki yake na alikufanya mshirika kwa kukuweka katika makao ya mbinguni nae. Wakati wewe kweli unajua na unaamini wewe ni nani na umehusishwa na nani, na utakataa kukubaliana na dhambi pamoja na matokeo yake. Sisi ni watendakazi pamoja na Mungu aliyetuumba kwa mfano wake na tumeumbwa kwa uzuri ili kutenda mema na kumuiga yeye. Wewe ni mtoto wa Mungu anayependwa sana. Leo, unawezaje kuondoa utambulisho wako katika Kristo kwa namna ya kumletea baba yako heshima?

Naweza Kuhusiana

Sijui kuhusu wewe, lakini siku ambazo nilihisi kama mtumwa ni wachache na mbali. Uchaguzi mbaya, majibu ya wazee kawaida na mara nyingi na ubinafsi wa wazi hunijaza majuto na kukata tamaa, na sijihisi kuwa mtumwa hata kidogo. Lakini ni nani au ni nini unachoenda kufuata na kuongozwa nacho? Adui ananong'oneza katika sikio lako ama neno la Mungu kupitia maandiko? Tatizo ambalo sote tunakabaliana nalo ni kwamba hisia zetu hushawishi mawazo yetu na mafikira yetu, ikiwa haijachukuliwa mateka, huongoza katika matendo ambayo tunakuja kujutia. Mara nyingi hii inachochea tu hisia ambazo tulifuata bila busara hapo mwanzo. Ninajua mimi ni kiumbe kipya, lakini ninatambua kuwa ninahitaji kufanya upya akili yangu kama ilivyo rahisi kutazama kwenye kioo na kutokubaliana na ukweli! Upya huu si wa mara moja lakini mchakato unaoendelea unaowezekana kwa neno lake, ambalo ni hai na linaishi. Kama vile gari linahitaji matengenezo ya mara kwa mara vivyo hivyo ninahitaji neno la Mungu kuendelea kufanya upya akili yangu. Na ninapofanya hivyo, hisia zangu, matukio na mtazamo wangu huanza kulinganishwa vizuri sana kama mtumwa ananiambia mimi ndiye.

Maswali

1. Je, unang'ang'ana kujiona kama mtumwa, na kama ni hivyo kwa nini?

2. Jadili hisia ambayo unakumbana nayo mara kwa mara inayosababisha majuto?

3. Unawezaje kuwa na mazoea zaidi ya kufanya upya akili yako?

Tafakari ya Maandiko

Warumi 6:15-23

Kipindi Cha 11

Uhusiano na Giza

Inaweza kutushawishi kulaumu mtu fulani, kitu fulani au hali fulani tunapofanya dhambi, lakini wakati chaguo letu la kutenda dhambi mara nyingi linapodhihirika na matokeo ya inje, hakuna yeyote anayetufanya tutende dhambi. Kila mara tunachagua kwa hiari yetu wenyewe. Tunaweza jaribu kugawanya dhambi zetu na hata tunaweza jaribu kusawazisha kile tunachofanya kwa kujaribu kujihakikishia kwamba pornografia tuliyo tazama ilikuwa picha au video ya nasibu tu, au tukio tulilokutana nalo usiku uliopita halijalishi lilikuwa uamuzi wa siku moja. Lakini tunaposhiriki katika dhambi ya asili ya ngono, si tu tendo la kihisia la tamaa kwa hakika ni tendo la uhusiano na yote ambayo ni machafu na yasiyo matakatifu. Kama waumini na watu wa Mungu tunapochagua kile ambacho ni kitakatifu na cha heshima, tunajenga uhusiano na Bwana na yote yaliyo matakatifu. Lakini tunapochagua dhambi kila mara ya asili chafu, tunamwalika adui kuja maishani mwetu na kuanzisha hatua mpya. Huu ndio tunaita uhusiano na giza. Adui anapobisha hodi kwenye mlango wa mioyo na akili zetu na kutupa jaribu la uhusiano wa uongo, tunahitaji kuchukua msimamo imara na kukataa kujihusisha na fursa za dhambi ambazo ni mbaya, uchafu, na kinyume na wito wa Mungu kwa utakatifu na haki. Pornografia, mafikirio yenye tamaa mbaya, usherati n.k, kufungua mioyo na akili zetu kuathiriwa na giza. Tangu mwanzo wa nyakati, dhambi imeahidi utoshelevu wa papo hapo, lakini ni utoshelevu wa udanganyifu ambao hautimii.

Nikikengeuso cha uharibifu na chombo kutoka kwa adui ambacho kwa ufanisi hutuvuta mbali kutoka kwa uhusiano wetu na Kristo. Tunapochagua mtazamo wa milele na wa kiungu unao tegemea neno la Mungu, mtazamo unaoona dhambi kuwa uchafu na kama tendo la uhusiano na giza, basi mvuto wa uhusiano wa uongo hupoteza mvuto wake. Shetani anaweza tu kupindisha kile ambacho Mungu anamaanisha kwa wema na anatamani kuzuia uhusiano wa kudumu na utimilifu ambayo Mungu anatamani kutupa sisi. Mungu alikuwa na mpango wa uhusiano tangu mwanzo kabisa na haukuhusisha kamwe uhusiano wa uongo na ufalme wa giza. Kwa nini tunaona ni rahisi sana kukimbilia kile ambacho ni kichafu na cha uongo? Hapa kuna sababu tatu za kawaida

- Ni vizuri na tumezoea mzunguko wa dhambi, kutubu, kurudia.
- Huenda kusiwe na matokeo ya mara moja au ya muda mrefu ambayo yanatuchochea kufanya mabadiliko ya kiungu.
- Tunajaribu kupuuza giza ambalo bado liko ndani ya mioyo yetu na dhamira zetu wenyewe.

Majaribu ya dhambi ni mbinu ya adui. Anaweza kukuvuruga, ili aweze kukudanganya, kwa lengo la kukuangamiza hatimaye. Kama biblia inavyosema katika Waefeso 4:27, “Msimpe adui nafasi.” Ingawa mstari huu unazungumza haswa kuhusu hasira, kanuni inaweza kutumika kwa ufatiliaji wetu wa usafi. Tunapaswa kuwa na hekima, kuwa macho, na kujiepusha na kumpa adui nafasi yoyote ya kuendesha katika mioyo, mawazo, au maisha yetu.

Tunaweza kujaribiwa kufikiria kwamba vita vyetu pamoja na majaribu na dhambi vinatoka kwenye chanzo kimoja tu -Ibilisi. Na ingawa hiyo ni kweli, pia kuna chanzo kingine ambacho tupo tunapigana vita nacho na hiyo ni vita ya mioyo yetu. Mungu anataka kufanya kazi ndani ya mioyo yetu na kutufanya upya (Zaburi 51:10, Wakolosai 3:10). Matendo yako yana yanalinganishwa na moyo wako, na yatakupeleka kwenye mtelezo kuelekea vilindi vya dhambi au kwenye hatua za usafi mkubwa. Ingawa chaguo la kuteleza linaweza kuwa rahisi, kupanda hatua kuelekea usafi mkubwa ndio njia sahihi ya kuchukua. Ingawa itahitaji juhudi nyingi kwa upande wako, hutajuta kamwe kuweka juhudi ili uweze kuelekea kwenye usafi mkubwa, ukamilfu, na kufanana na Kristo. Maamuzi ya busara ambayo ni matakatifu na heshima si ya mitume tu au watu wakuu wa imani wazamani. Ni za kila mtu pamoja na wewe. Katika ulimwengu wetu wa leo, kwa kawaida kuna ufafanuzi mmoja tu mkuu wa uhusiano na unaeleweka ndani ya mkutadha wa tabia ya ngono. Ingawa uhusiano mara nyingi hufikiwa kuwa wa kufungiwa kwenye kitanda cha ndoa (au kukutana na ukosefu wa adili) unapaswa pia kuona kuwa sehemu yenye afya na muhimu ya uhusiano wetu wa karibu ambao uaminifu, udhaifu, usikivu, huruma na utunzaji ndio msingi. Mungu alituumba ili tuwe na uhusiano naye kwanza kabisa kisha tuwe na mahusiano sahihi na matakatifu kati yetu sisi wenyewe.

Sehemu ya kufuatilia usafi na utimilifu ni kujifunza jinsi ya kufuata uhusiano katika mahusiano ambayo ni kama ya Kristo, yasiyo na ubinafsi, na yanayotegemea mifano inayopatikana katika neno la Mungu. Tunaamini kuwa wakati wanaume wana uhusiano wa karibu kama huo pamoja na ndugu wengine Wakristo, badala ya kufuatilia uhusiano na giza tunapitia kiwango cha uhusiano ambao ni wa utakatifu, na wa kibiblia, usio na ngono, na unaotoa maisha kwa roho zetu. Kama watu wa Mungu, ni lazima tustawishe maana ya mahusiano ya kumheshimu Mungu pamoja na ndugu waliozungumziwa tunaposoma maandiko yafuatayo: “Rafiki hupenda nyakati zote, na ndugu amezaliwa wakati wa taabu” Methali 17:17 (NIV) “Mtu aliye na marafiki wasio waaminifu huangamia upesi, lakini yuko rafiki anayeshikamana na mtu kuliko ndugu.” Methali 18:24 (NIV) “Naye Yonathani akafanya agano na Daudi kwa sababu alimpenda kama nafsi yake.” 1 Samweli 18:3 (NIV) Sisi sote tunapaswa kuwa na ndugu ambaye tunaweza kuwa waaminifu kwake sote. Tunapaswa kuwa na ndugu ambaye hatatukimbia wakati upungufu umeonyeshwa. Sote tunahitaji kuwa na ndugu tunayeweza kumwamini ili kutembea nasi katika safari hii ya maisha na sio wakukimbia kwa dalili za kwanza za shida au usumbufu. Sote tunahitaji ndugu ambaye atatusikia kwa sababu anafahamu maisha si tu kurekebisha shida za mwingine. Sote tunahitaji kuwa na ndugu ambaye tunajua kuwa anajali kutuhusu. Si kwa kawaida “habari yako leo?” kupitia maoni, lakini aina ya huduma ambayo inachukua mkono wetu na kuinua juu tunapoanguka, si mara moja tu, lakini mara kwa mara. Leo, unawezaje kuimarisha uhusiano wako na Mungu na wengine kupitia uaminifu zaidi, udhaifu, usikivu na huruma?

Naweza Kuhusiana

Nina uhakika umesikia hadithi kuhusu chura ambaye kwa polepole alichemshwa hai. Msingi ni kwamba ikiwa chura atawekwa ghafla kwenye maji yanayochemka ataruka inje; lakini ikiwa chura atawekwa kwenye maji ya vuguvugu ambayo yanachemshwa kidogo kidogo, hataona hatari na atapikwa polepole hadi kufa. Adui anafanya vivyo hivyo na sisi. Kwangu mimi ilianza na mazoea yangu ya pornografia, tabia ambayo ningehalalisha kwa kusawazisha kwamba hakuna mtu mwingine aliyehusika na sikua nikimuumiza yoyote. Lakini nikishindwa kutambua kwamba vile 1 Yohana 5 ni kweli na Mungu ni nuru na ndani yake hamna giza hata kidogo, hivyo ni kweli kwamba nilipoingia ndani na giza, Mungu hakua ndani yangu, na maji yalipozidi kuwa moto tabia yangu ya pornografia ilizidi kuwa nyeusi, kutoka kwa kusimama usiku moja na kuwa na makahaba. Bila upendo wa ndugu wa kunisaidia kutoka kwenye chungu, ningeendelea kwenye njia inayoongoza kwenye kifo. Kutambua ni alama unapoanza kuhalalisha chaguo lako na kukimbilia mlango wa ushirika na uhuru

Maswali

1. Ni kwa njia gani mara nyingi unahalalisha uchaguzi mbaya?

2. Je, chaguzi hizi zina athirije matembezi yako na Mungu?

3. Je, ni hatua gani unaweza kuchukua ili kusaidia kutembea katika nuru mfululizo zaidi?

Tafakari ya Maandiko

1 Petro 1:13-16

Kipindi Cha 12

Maeneo ya Kijivu

“Upambanuzi sio tu swala la kutofautisha lililo sawa na lisilo sahihi; bali ni tofauti kati ya haki na karibu sawa” - Charles Spurgeon

Sote tuna maeneo katika maisha yetu ambapo tunajihusisha kwa hiari katika nyenzo zenye kutiliwa shaka ambazo hatimaye hutuongoza kwenye njia ya maelewano ya dhambi na majuto ya dhati. Mojawapo ya njia ya kawaida na za hila ambazo tunaishia kuchagua dhambi ni kwa kugawanya majaribu katika maeneo ya kijivu na maeneo nyeusi. Unaweza kujiuliza, “maeneo ya kijivu na nyeusi ni nini?” Hebu tuanze na kuelewa nini eneo nyeusi. Eneo nyeusi haliachi nafasi kwa mtu kusema, “Nimejikwaa juu ya hili” eneo jeusi ni wazi tovuti za pornografia, programu za kuunganisha, video na majarida ya ngono na nyenzo za usherati miongoni mwa mambo mengine. maeneo nyeusi ni yenye dhambi, na tunahitaji kuzikimbia fursa kama hizo zinapojitokeza kwetu. Sasa hebu tuelewe ni nini eneo la kijivu. Eneo la kijivu haliwezi kuwa na dhambi waziwazi. Bado, ni eneo ambalo hatimaye litakuongoza kuelekea mambo maovu ambayo unajua hupaswi kuyafikiria au kuyafanya. Eneo la kijivu litasababisha mjadala wa ndani na kukadiria hekima ya hatua yako na uwezo wa kupanda mbegu ya shaka na kuhesabiwa haki ambayo itakuongoza kwenye maelewano. Wakati maeneo ya kijivu ni ya kibinafsi na yanatofautiana kutoka kwa mtu hadi mtu, kila mtu ana maeneo ya kijivu. Ili kuiweka kwa urahisi, maeneo ya kijivu ni upotovu wa udadisi wetu. Moja ya majaribu makubwa tutakayokumbana nayo ni mahali pa kuelekeza udadisi wetu. Lakini mara nyingi, tunajaribu kuhalalisha udadisi usiofaa na uchunguzi wa maeneo ya kijivu kwa kuja na kisingizio baada ya kisingizio..

Visingizio kama vile “nitaacha kabla halijawa mbaya”, nashangaa ni nini kipya? Ni mtazamo wa haraka tu au “sio mbaya vile, nimeona mbaya zaidi.” Tunapoweka mipaka yetu kuwa huru kiasi kwamba tunakiuka mipaka hiyo mara kwa mara, tunashindwa kuona udadisi wa dhambi unaoelekezwa kwenye maeneo ya kijivu kama kitu cha kuepukika. Iwapo unataka kuona ushindi maishani mwako utahitaji kutambua kwamba udadisi kuelekea dhambi huja na mipango yako ya uongo. Uongo unaojaribu kukushawishi kuwa kutakuwa na matokeo machache ya kuchunguza udadisi wako, ikiwa kuna yeyote. Uongo unaosema hakuna mtu atakaye umia mradi tu hakuna anayejua. Uongo unaosema kuwa una nguvu za kutosha kuacha, ingawa historia inakukumbusha kuwa mara chache hufanya hivyo.

Uongo ambao kwa namna fulani, kwa njia nyingine ungehalalisha uchunguzi wa ajabu wa dhambi. Udadisi juu ya maeneo ambayo yako kwenye mpaka wa dhambi (maeneo ya kijivu) hatimaye itakuongoza kwenye maeneo ambayo ni dhambi wazi (maeneo meusi).

Ingawa tunaweza kukubaliana kuwa udadisi ndani na yenyewe sio mbaya, tungependa uone kwamba mahali unapoelekeza udadisi wako ndio utakaoamua njia ambayo utapitia. Unaweza kujiambia, “udadisi haukuongoza kwenye dhambi wakati huu.” Hata hivyo lengo lako kama muumini sikuona ni mara ngapi unaweza kujiingiza kwenye dhambi bila kutenda dhambi.

Ukweli ni kwamba ingawa udadisi hauwezi kusababisha dhambi wakati huu kwa hakika utafanya wakati fulani. Mwanzo 4:7 ni ukumbusho mzuri kwetu sisi sote. “Ukitenda lililo sawa hautakubaliwa? Lakini usipotenda lililo sawa, dhambi inakuotea mlangoni nayo inakutamani, lakini lazima uishinde.”

